# IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

# MWONGOZO WA KITAIFA WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASILIMALI ZA UVUVI NA MAZINGIRA, TANZANIA

## IMEANDALIWA NA WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI

## FEBRUARI, 2017

# YALIYOMO

**VIFUPISHO** ........................................................ **v**
**KAULI YA WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI** ........ **vi**
**DIBAJI** ........................................................ **viii**
**SHUKRANI** ........................................................ **x**
1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1
1.1 Historia ya Usimamizi wa Uvuvi Nchini ........................ 2
1.2 Rasilimali za Uvuvi Tanzania ........................................ 4
1.3 Mchango wa Sekta ya Uvuvi ........................................ 4
1.4 Lengo la Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi ................ 5
1.5 Dhana ya Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi ...................... 6
1.6 Misingi ya Usimamizi Shirikishi ...................................... 6
1.7 Umuhimu wa Usimamizi Shirikishi ................................ 9

**2.0 MFUMO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASILIMALI ZA UVUVI** ........................................ **11**
2.1 Wadau na Majukumu yao katika Usimamizi Shirikishi ........... 12
2.1.1 Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi ......... 13
2.1.2 Serikali za Vijiji/Mitaa ........................................ 15
2.1.3 Mamlaka za Serikali za Mitaa ........................................ 16
2.1.4 Sekretariet za Mikoa ........................................ 17
2.1.5 Ofisi ya Rais TAMISEMI ........................................ 17
2.1.6 Wizara yenye dhamana ya Uvuvi ........................................ 18
2.1.7 Wadau wa Maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali .................. 19
2.2 Mahusiano na Mawasiliano Miongoni mwa Wadau ................ 20

**3.0 TAASISI YA USIMAMIZI SHIRIKISHI KATIKA** NGAZI YA JAMII ........................................ 21
3.1 Vikundi vya Usimamizi Shirikishi ........................................ 22
3.2 Muundo wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) ........................................ 22

3.3. Vyombo Vikuu vya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi ............. 23
3.3.1 Mkutano Mkuu ............................................................... 23
3.3.2 Kamati Tendaji................................................................ 24
3.3.3 Kamati ndogo:................................................................ 26
3.4 Majukumu na Wajibu wa Viongozi wa BMU ............................ 28
3.4.1 Mwenyekiti wa BMU........................................................ 28
3.4.2 Katibu wa BMU ............................................................... 28
3.4.3 Mweka hazina ................................................................. 29
3.4.4 Boharia ......................................................................... 29
3.4.5 Mzee Maarufu naanayekubalika............................................ 30
3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji Fedha na Matumizi .......................... 30
3.5.1 Ukusanyaji wa Fedha......................................................... 30
3.5.2 Matumizi ya Fedha ........................................................... 30
3.6 Ukomo wa Uanachama wa BMU.............................................. 31

4.0 MCHAKATO WA UANZISHAJI WA BMU ............................... 33
4.1 Mahali na Eneo la Utawala wa BMU........................................ 34
4.2 Hatua za Kuanzisha BMU...................................................... 35
4.2.1 Hatua ya kwanza: Kujenga uelewa na kukuza mwamko wa jamii ............................................................... 35
4.2.2 Hatua ya pili: Uchaguzi wa Viongozi wa BMU.......................... 35
4.2.3 Utaratibu wa Kuandaa Katiba ya BMU .................................... 38
4.2.4 Hatua ya Tatu: Kusajili BMU na kufungua Akaunti ................. 39

5.0 UENDESHAJI WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA UVUVI................................................................................ 40
5.1 Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi (CFMA)....................... 41
5.2 Utaratibu wa kufuata katika kuanzisha Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Uvuvi ............................................ 41
5.2.1 Hatua ya Kwanza: Utafiti shirikishi wa uvuvi wa eneo linalotarajiwa kusimamiwa............................................... 41

5.3.2 Hatua ya Pili: Mashauriano na Uhamasishaji ........................... 42
5.3.3 Hatua ya Tatu: Uanzishaji wa Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi ........................................................................... 43
5.3.4 Hatua ya Nne: Kutengeneza Mpango wa Usimamizi ................. 44
5.3.5 Hatua ya Tano: Kuomba Ridhaa kwa Mkrugenzi wa Uvuvi ........ 44
5.4 Uratibu wa Kitaasisi katika Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi ........................................................................... 45
5.5 Kamati ya Uratibu ........................................................................... 47
5.6 Uchaguzi wa Uongozi wa Kamati ya Uratibu ............................ 48
5.7 Kazi za Kamati ya Uratibu ........................................................ 48
5.8 Utaratibu wa usimamizi wa uvuvi ndani ya Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja ........................................................ 49
5.8.1 Utayarishaji wa Mpango wa Usimamizi ................................... 49
5.8.2 Utayarishaji wa Mpango kazi .................................................. 50
5.9 Usimamizi wa Makambi (Madago) ya Uvuvi ............................ 50

**6.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI .................................... 51**
6.1 Ngazi za ufuatiliaji ........................................................................... 51
6.2 Maeneo Makuu ya Viashiria vya Ufuatiliaji .............................. 52
6.3 Njia za ufuatiliaji ........................................................................... 52
6.4 Tathmini ........................................................................................ 53
6.5 Matokeo ya Tathmini .................................................................. 54
6.6 Ufuatiliaji na Tathmini wa Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja ........................................................................................ 57
6.6.1 Madhumuni ya Ufuatiliaji na Tathmini ................................... 57
6.6.2 Ufuatiliaji na Tathmini ............................................................. 58
6.6.3 Ufuatiliaji wa hali ya rasilimali ................................................ 60
6.6.4 Kutoa Ripoti ................................................................................ 61

**6.7 UTAFITI ........................................................................ 61**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BMUs | Beach Management Units (Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi) |
| CFMAs | Collaborative Fisheries Management Areas (Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Uvuvi) |
| FETA | Fisheries Education and Training Agency (Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi) |
| MPRU | Marine Parks and Reserves Unit (Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu) |
| LVEMP | Lake Victoria Environment Management Programme (Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria) |
| TAFIRI | Tanzania Fisheries Research Institute (Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania) |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |

# KAULI YA WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inalo jukumu la kuhifadhi, kulinda, kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi hapa nchini na kuhakikisha kuwa Sekta ya Uvuvi inachangia kikamilifu katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Taifa. Katika kutekeleza wajibu huu pamoja na kufikia malengo tarajiwa, Wizara inalo jukumu la kuandaa sera, sheria, kanuni za uvuvi pamoja na miongozo mbalimbali kwa lengo la kusimamia Sekta ya Uvuvi. Usimamizi wa uvuvi, nchini unaongozwa na Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 ambazo zinahimiza umuhimu wa jamii kushirikishwa katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi. Dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi inalenga kushirikisha wadau wa uvuvi hasa jamii za wavuvi katika kutekeleza majukumu ya usimamizi ili kuimarisha uvuvi endelevu.

Usimamizi wa rasilimali za uvuvi unakabiliwa na changamato mbalimbali ikiwa ni pamoja na ushiriki usioridhisha wa jamii katika kulinda, kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi. Hali hii imesababisha upungufu wa rasilimali za uvuvi, kuchochea uvuvi haramu, uharibifu wa mazalia ya samaki na mazingira yake na hivyo Sekta ya Uvuvi kushindwa kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa. Aidha, uzoefu unaonyesha kuwa dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi imekuwa ikitumika na mataifa ya Asia na Ulaya na mataifa machache ya Afrika yameanza kupata mafanikio makubwa.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inatambua umuhimu wa kuishirikisha jamii ya wavuvi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake ambapo Wizara imeanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (Beach

Management Units – BMUs). Katika kuhakikisha kuwa jamii inashirikishwa kikamilifu, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira kwa lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinakuwa endelevu na hivyo Sekta ya Uvuvi kuwa na tija na kuchangia ipasavyo katika Pato la Taifa na jamii za wavuvi kwa ujumla.

Wizara inatoa rai kwa jamii kutumia mwongozo huu ili kushiriki kikamilifu katika kusimamia rasilimali za uvuvi ambazo ni muhimu kwa Taifa.



.............................................

Dkt. Charles J. Tizeba (Mb)
Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi

# DIBAJI

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la WWF Ofisi ya Tanzania (World Wide Fund for Nature -WWF) inatekeleza shughuli za kusimamia, kuhifadhi, kulinda na kuendeleza rasilimali za uvuvi kwa ajili ya kupunguza umasikini na kuleta maendeleo kwa jamii za wavuvi na wananchi kwa jumla nchini. Kutokana na changamoto za usimamizi wa rasilimali za uvuvi, Wizara (Idara ya Maendeleo ya Uvuvi) imebaini kwamba kuna umuhimu wa kuwa na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na hivyo imejumuisha dhana ya ushirikishwaji katika Sera, Sheria na Kanuni za uvuvi.


Katika kutekeleza dhana ya ushirikishwaji, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, imeanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi vinavyofahamika kama "Beach Management Units – BMUs". Ili kuwa na Vikundi vyenye ufanisi na tija, Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi. Lengo la mwongozo huu ni kuiwezesha Serikali Kuu,Mamlaka za Serikali za Mitaa, jamii ya wavuvi, na wadau wengine kushirikiana katika kusimamia, kulinda, kutunza, kuendeleza na kuvuna kwa busara rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kiuchumi, ajira, bioanuai, uhakika wa chakula kwa taifa kwa kuzingatia Sera na Sheria za uvuvi zilizopo.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wizara na Taasisi za Serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa, mashirika ya kiraia, sekta na watu binafsi.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Idara ya Maendeleo ya Uvuvi) itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa

mwongozo huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ni matumaini ya Wizara kuwa Mwongozo huu utatumika kama ulivyokusudiwa na hivyo kuwezesha dhana ya Usimamizi Shirikishi kuleta ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazingira nchini. Hii itawezesha kuwepo kwa rasilimali za uvuvi na uvuvi endelevu hivyo kuinufaisha jamii na nchi kwa ujumla.



.................................
Dkt. Yohana L. Budeba
Katibu Mkuu - Uvuvi
Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Februari, 2017

# SHUKRANI

Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi inatoa shukrani za dhati kwa TAFIRI, MPRU, FETA, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shirika la WWF Ofisi ya Tanzania “World Wide Fund for Nature (WWF)”, Sea Sense, Tanzania Nature Conservance , Tanzania Tuna Fishery National Alliance, Tanzania Fisheries and Aquatic Organization kwa kushiriki katika mchakato wa kuandaa mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi nchini. Aidha, shukrani za dhati zinatolewa kwa Shirika la WWF Ofisi ya Tanzania na Mradi wa SWIOFish kwa kuwezesha kazi hii kufanyika hadi kukamilika kwa Mwongozo. Pia, Wizara inawashukuru wadau wote ambao kwa njia moja au nyingine walichangia katika utayarishaji wa mwongozo huu. Michango ya maoni na ushauri waliotoa katika kuandika mwongozo huu unathaminiwa.

Aidha, Wizara inatambua ushiriki wa Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika, Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) na wataalam wa kujitegemea katika kuhakikisha kuwa kazi hii inakamilika. Kukamilika kwa Mwongozo huu kutaimarisha ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi na utekelezaji wake utawezesha rasilimali za uvuvi kuwa endelevu na hivyo kuongeza tija na kuchangia kikamilifu katika Pato la Taifa na kuongeza kipato cha jamii.

# 1.0 UTANGULIZI

Sekta ya Uvuvi inaongozwa na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 yenye lengo kuu la kuendeleza Sekta ya Uvuvi ili iwe yenye ushindani na ufanisi katika kuchangia kwenye uhakika wa chakula, lishe na ukuaji wa uchumi wa taifa pamoja na kuboresha ustawi wa wadau wa uvuvi kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Ili lengo hili liweze kutekelezeka Serikali inaendelea kudumisha ushirikiano wa kiutendaji na wadau wengine ambao kwa njia moja au nyingine wanahusika katika kulinda, kusimamia na kutumia rasilimali hizo kwa busara. Wadau hao ni pamoja na jamii ya wavuvi, sekta binafsi, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Vyuo Vikuu, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI), Kitengo cha Hifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya dini na wadau mbalimbali wa maendeleo. Usimamizi wa majukumu haya unafanyika kwa kutumia Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015, sheria na kanuni za uvuvi pamoja na miongozo iliyopo.

## 1.1 Historia ya Usimamizi wa Uvuvi Nchini

Kabla ya ukoloni usimamizi wa uvuvi ulifuata mifumo ya jadi (utamaduni, mila na desturi) ya jamii husika. Jamii ilikuwa inamiliki rasilimali za uvuvi ambapo kwa kiasi kikubwa viongozi wa jadi walikuwa na mamlaka ya kudhibiti utumiaji wa rasilimali hizo. Hivyo, jukumu la usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulikuwa mikononi mwa jamii. Aidha, katika mifumo hiyo ya jadi, kulikuwa na uhusiano baina ya jamii katika usimamizi wa raslimali za uvuvi.

Wakati wa ukoloni, mfumo wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi wa jadi uliokuwa na msingi wa umiliki wa jamii ulibadilika na nafasi yake kuchukuliwa na mfumo wa usimamizi wa kikoloni ambapo usimamizi wa rasilimali za uvuvi ulitawaliwa na sheria ya kikoloni kwa maslahi ya wakoloni (Fisheries Ordinance Cap. 295 and The Trout Protection Ordinance, Cap 368).

Baada ya uhuru, Serikali ilianzisha Idara ya Uvuvi mwaka 1965 chini ya Wizara ya Ardhi, Misitu na Wanyama. Serikali ilitunga Sheria ya Uvuvi Na. 6 ya mwaka 1970 ili kusimamia rasilimali za uvuvi, ingawa jukumu la usimamizi wa rasilimali za uvuvi lilionekana kama ni la watumishi wa Serikali pekee. Aidha, Kutokana na ukuaji wa Sekta ya Uvuvi na changamoto zake mwaka 1997 Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Sekta ya Uvuvi na Mikakati yake ambayo ilitambua umuhimu wa jamii kushiriki katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

Katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Sekta ya Uvuvi na Mikakati yake ya Mwaka 1997, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Na. 6 ya Mwaka 1970 na kupatikana kwa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za 2005. Aidha, Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2005 zilizofanyiwa marekebisho na kupatikana kwa Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009. Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 zilitambua ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia rasilimali za uvuvi kupitia mfumo wa uanzishwaji wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi vinavyofahamika kama “Beach Management Units - BMUs”.

Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi Tanzania ulianza miaka ya 1990 katika Ziwa Victoria kwa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi vilivyojulikana kama BMUs chini ya Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria (LVEMP). Hata hivyo, BMUs hizo ziliundwa bila kuwa na sheria wala mwongozo. Baada ya kutungwa kwa Sheria ya Uvuvi ya Mwaka 2003, miongozo ya Usimamizi Shirikishi katika Ziwa Victoria na Ukanda wa Pwani iliandaliwa na kutumika. Usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi unatarajiwa kuziwezesha jamii za wavuvi kutekeleza kisheria, haki na wajibu wao wa kusimamia rasilimali za uvuvi ili kuongeza tija na kipato.

## 1.2 Rasilimali za Uvuvi Tanzania

Tanzania ina maeneo mengi ya maji baridi na maji bahari, yenye rasilimali nyingi za uvuvi ambamo shughuli za uvuvi hufanyika. Ukanda wa Pwani una urefu wa kilometa 1,424. Eneo la bahari lina upana wa maili za majini 200 (12 Maji ya Kitaifa na 188 ni Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari) sawa na kilometa za mraba 287,000 (64,000km2 Maji ya Kitaifa na 223,000km2 Ukanda wa Kiuchumi wa Bahari).

Eneo la maji baridi linajumuisha maziwa makuu matatu ambayo ni Victoria lenye kilometa za mraba 68,800 ambapo Tanzania inamiliki asilimia 51 sawa na kilometa za mraba 35,088; Tanganyika lenye kilometa za mraba 32,900 ambapo Tanzania inamiliki asilimia 41 sawa na kilometa za mraba 13,489 na Ziwa Nyasa lenye kilometa za mraba 30,800 na Tanzania inamiliki asilimia 18.51 sawa na kilometa za mraba 5,700.

Pia, kuna maziwa madogo yanayojumuisha Ziwa Rukwa, Manyara, Babati, Basutu, Eyasi, Kitangiri, Burigi, Duluti, Jipe, Chala, Ikimba, Singidani, Momela, Nguruka, Kindai, Natron, Katwe, Rwakajunju, Merule, Kalenge, Mitoma, Ngoma, Tlawi, Hombolo, Lwambahili na Rushwa.

Maeneo mengine ni pamoja na Mto Rufiji, Ruvuma, Wami, Pangani, Ruvu, Kagera, Malagarasi, Kilombero, Ruaha, Mara, Lukuledi, Matandu, Mbwemkuru, Umba, Songwe na maeneo oevu yanayojumuisha Malagarasi na Bahi. Pia, kuna mabwawa ya Nyumba ya Mungu, Mtera, mabwawa ya asili na malambo.

## 1.3 Mchango wa Sekta ya Uvuvi

Sekta ya Uvuvi huchangia katika uhakika wa chakula, lishe, ajira, kipato, ukuaji wa uchumi wa Taifa pamoja na kuboresha ustawi wa

wadau wa uvuvi kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Sekta hii huajiri takriban wavuvi wanaojihusisha na uvuvi moja kwa moja wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 183,800 pamoja na wananchi wengine wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 4,000,000 (Sera ya Uvuvi Mwaka, 2015) wanaojishughulisha kwenye Sekta ya Uvuvi kwa kufanya biashara ya samaki, uchakataji wa samaki na mazao mengine ya uvuvi, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi, biashara ndogondogo na mama lishe.

Vile vile, sekta huchangia takriban asilimia 30 ya ulaji wa protini itokanayo na wanyama. Aidha, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.3 na kuchangia asilimia 1.4 mwaka 1998 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na mwaka 2014 ambapo sekta ilikua kwa kiwango cha asilimia 5.5 na kuchangia asilimia 2.4 katika Pato la Taifa (Sera ya Uvuvi Mwaka, 2015).

Rasilimali za uvuvi zimeendelea kupungua kutokana na ongezeko la idadi ya wavuvi, vyombo na zana za uvuvi (nguvu ya uvuvi) pamoja na matumizi ya mbinu na zana haribifu. Hali hiyo imesababisha kupungua kwa upatikanaji wa samaki kwani wavuvi wamekuwa wakivua katika maeneo ya karibu na fukwe ambayo ni mazalia na makulia ya samaki. Hivyo, ni muhimu kuimarisha usimamizi kwa kushirikiana na wadau wa uvuvi kwa kuwa na Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi. Maandalizi ya Mwongozo huu yamezingatia michango ya wadau mbalimbali, taratibu zilizopo na hali halisi ya rasilimali za uvuvi nchini.

## 1.4 Lengo la Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi

Lengo la mwongozo huu ni kuiwezesha Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, jamii ya wavuvi na wadau wengine kushirikiana katika kusimamia, kulinda, kutunza, kuendeleza na kuvuna kwa busara rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya kiuchumi, ajira, bioanuai,

uhakika wa chakula kwa taifa kwa kuzingati sera na sheria za uvuvi zilizopo.

## 1.5 Dhana ya Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi

Dhana ya usimamizi shirikishi inalenga kushirikisha wadau mbalimbali katika kupanga, kuamua, kuhifadhi, kusimamia na kutumia kwa busara rasilimali za uvuvi na mazingira yake ili kuwa na rasilimali endelevu zenye tija. Usimamizi shirikishi umekuwa ukitumika kama njia ya kuboresha ufanisi wa usimamizi wa uvuvi, na kwa kutambua kwamba ushirikishwaji wa watumiaji wa rasilimali katika usimamizi utaboresha uelewa, umiliki na dhamira.

## 1.6 Misingi ya Usimamizi Shirikishi

Uzoefu wa kimataifa umeonesha kuwa mafanikio katika usimamizi shirikishi wa uvuvi yametokana na uelewa wa changamoto zinazokabili usimamizi wa rasilimali za uvuvi pamoja na kuwahamasisha wadau wa uvuvi kusimamia uvuvi kikamilifu. Aidha, maeneo ambayo usimamizi shirikishi umeshindwa kufanikiwa umetokana na watumiaji wa rasilimali kutojua matatizo yanayoikabili rasilimali hiyo. Changamoto za usimamizi wa rasilimali za uvuvi ni pamoja na kuendelea kupungua kwa samaki wanaovuliwa, upotevu wa aina muhimu za samaki, uharibifu wa mazingira (kama vile kukata mikoko), na kuwepo kwa migogoro ya matumizi ya rasilimali.

Ili kufanikisha usimamizi shirikishi ni muhimu kuzingatia misingi ifuatayo: -

### a) Umiliki na uwajibikaji

Ili dhana ya usimamizi shirikishi iweze kutekelezwa kikamilifu, jamii inatakiwa kuelewa kuwa wao ndiyo wamiliki wa rasilimali

hizo. Hivyo jamii inatakiwa kuwajibika kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

### b) Uongozi imara

Uongozi ni msingi muhimu katika usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi hasa katika ngazi za vijiji/mtaa ambako rasilimali inapatikana. Ili kufikia malengo ya usimamizi shirikishi viongozi wanatakiwa watokane na watumiaji wa rasilimali au makundi ambayo yako mstari wa mbele kulinda rasilimali za uvuvi. Mafunzo na elimu ni muhimu katika upatikanaji wa viongozi madhubuti katika usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi.

Wakati wa kuanzisha usimamizi shirikishi, inashauriwa kwamba ni vyema kufahamu mifumo na miundo ya uongozi katika jamii husika, uelewa wa jamii katika kuheshimu makundi mbalimbali ya jamii, tabia za vikundi na changamoto zake, na pia kuchunguza utamaduni na uchumi wa jamii za wavuvi katika eneo husika.

### c) Ushirikishwaji wa Wadau

Ni muhimu kutambua kuwa wadau wa usimamizi shirikishi sio wale tu walioko karibu na rasilimali (watumiaji wa rasilimali – wavuvi). Wadau ni pamoja na taasisi, makundi ya kijamii na watu/vikundi vilivyo na majukumu ya moja kwa moja katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi wa eneo husika. Ushirikishwaji wa wadau wote bila kujali itikadi zao katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaongeza ufanisi katika usimamizi na unapunguza migogoro na gharama za usimamizi. Pia, unaongeza ufanisi wa ukusanyaji wa taarifa za uvuvi. Hivyo, ni vyema kufanya na kutathmini aina za wadau ambao hubadilika kila

wakati kwa vile matumizi na mahitaji ya rasilimali hubadilika pia.

### d) Kujenga uwezo wa wadau

Katika utekelezaji wa dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi ni muhimu kuiwezesha jamii kupanga na kutoa maamuzi ya maendeleo ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kuongeza tija na hatimaye kuboresha maisha yao. Hatua hii inaiwezesha jamii kutekeleza mipango ya maendeleo kwa kuzingatia rasilimali wanazomiliki na hivyo kuwezesha usimamizi makini. Uwezeshaji pia unalenga kuwatambua watumiaji halisi wa rasilimali za uvuvi, mipaka halisi ya usimamizi wa rasilimali pamoja na sheria na kanuni za usimamizi wa rasilimali.

### e) Mahusiano baina ya Wadau

Ili utaratibu wa usimamizi shirikishi uweze kudumu ni lazima kudumisha uhusiano, uaminifu na kuheshimiana kati ya washirika. Kujenga kuaminiana kati ya washirika kunachukua muda mrefu na jitihada za kujenga uaminifu baina ya washirika zinahitajika. Uwazi, ushirikishwaji, nidhamu, utii na uadilifu pia vinapaswa kudumishwa. Aidha, ni muhimu kujenga na kuimarisha mitandao katika usimamizi wa rasilimali ili kuwezesha wadau kuwa na taarifa na uzoefu katika kuwezesha usimamizi shirikishi kwa ufanisi zaidi. Ujenzi wa mtandao wa mashirika/vikundi vya kijamii ni dhana yenye nguvu kwa ajili ya upashanaji habari, uwezo wa kujifunza mbinu mbalimbali zinazofanywa na vikundi vingine, kukuza ushirikiano pale nguvu ya pamoja inapohitajika na kuimarisha juhudi za pamoja. Pia, uanzishaji wa mitandao husaidia kutumia rasilimali kwa uangalifu kama vile rasimali watu, fedha na gharama za usafiri na usafirishaji.

### f) Utulivu wa Kijamii

Usimamizi imara wa rasilimali za uvuvi unachangiwa na hali ya utulivu katika jamii. Hali hii husaidia jamii kujenga maisha yao pasipo kuwa na vurugu katika usimamizi wa rasilimali zao.

### g) Mawasiliano

Kuwepo vikao kwa ajili ya majadiliano ili kuelewa mahitaji na matarajio ya wadau wote ni miongoni mwa mambo muhimu katika usimamizi shirikishi. Mijadala ya wadau wote iliyo huru na wazi inahitajika ili kubadilishana taarifa na hivyo kujenga mawasiliano imara. Pamoja na mambo mengine, mijadala itasaidia kupanua ufahamu wa mahitaji, majukumu, wajibu miongoni mwa wadau, pamoja na faida na gharama zinazotarajiwa katika muda mfupi na muda mrefu.

### h) Udhibiti wa migogoro

Katika usimamizi shirikishi, usuluhishi na utatuzi wa migogoro ni muhimu ufanyike wakati inapotokea. Kama kutatokea migogoro miongoni mwa watumiaji wa rasilimali za uvuvi jukwaa la wadau wa sekta ya uvuvi litatumika kujadili na kutatua migogoro katika ngazi mbalimbali (Vijiji, Kata, Wilaya na hata Taifa).

## 1.7 Umuhimu wa Usimamizi Shirikishi

Serikali kwa kushirikiana na wadau ina jukumu la kuhakikisha kuwa rasilimali za uvuvi zinalindwa, zinatunzwa, zinahifadhiwa na kutumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Dhana ya usimamizi shirikishi katika usimamizi wa raslimali imekuwa ikitumika katika nchi mbalimbali duniani kama vile nchi za Philippine, Ghana na Madagascar ambapo imeonesha mafanikio.

Sekta ya Uvuvi inakabiliwa na changamoto nyingi zinazohusiana na usimamizi na uvuvi endelevu wa rasilimali za uvuvi zikiwemo: upungufu wa rasilimali za uvuvi, uvuvi haramu, udhaifu katika usimamizi, kutoweka kwa baadhi ya aina ya rasilimali za uvuvi, ukosefu wa vitendea kazi, elimu duni ya usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na matumizi duni ya teknolojia za kisasa, ongezeko la watumiaji wa rasilimali za uvuvi pamoja na uharibifu wa bioanuai na mazingira. Katika kukabiliana na changamoto hizo, katika miaka ya hivi karibuni, Serikali iliamua kushirikisha jamii katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kuanzisha Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) kwa lengo la kuimarisha usimamizi.

Kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa shughuli za BMUs zikiwemo muundo wa BMUs, uelewa mdogo kuhusu usimamizi shirikishi, uvuvi haramu, ukosefu wa rasilimali fedha na vitendea kazi pamoja na BMUs nyingi na baadhi ya wadau kutotambua au kutekeleza majukumu yao. Mwongozo huu umekusudia kuzifanya BMUs kupata nguvu za kiuchumi, kisheria na kiutawala zaidi kuliko hapo awali ambapo wanachama wa BMUs watapaswa kutoa ada ya uanachama, kiingilio na kubuni vyanzo vingine ili kufanya BMUs kuwa na fedha za kujiendesha.

Katika mwongozo huu, BMUs zilizoanzishwa au zitakazoanzishwa katika ngazi ya kijiji zitapaswa kutimiza masharti yafuatayo;

i) Kuwa na Katiba;
ii) Kuhakikisha inapata usajili kutoka kwa mamlaka husika;
iii) Kutambuliwa na kukubalika na uongozi wa Kijiji/Mtaa husika

# 2.0 MFUMO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASILIMALI ZA UVUVI

## 2.0 MFUMO WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASILIMALI ZA UVUVI

Mfumo wa usimamizi shirikishi uliopo Tanzania unasimamia kwenye misingi ya Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015. Sera hiyo inatambua na kuhamasisha ushiriki wa Serikali pamoja na jamii katika kusimamia rasilimali za uvuvi. Ugatuaji wa madaraka unapelekea utekelezaji wa usimamizi shirikishi wa uvuvi kuongozwa na taasisi kuu mbili za Serikali, ambazo ni TAMISEMI na Wizara yenye dhamana ya Uvuvi. Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 inataja dhana ya ugatuaji wa madaraka kama njia inayofaa kusimamia masuala ya uvuvi, kwa vile itawezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia rasilimali za uvuvi na mazingira yake kwa kutumia mifumo shirikishi ya kijamii. Sambamba na Sera ya Uvuvi, Sheria ya Uvuvi na Kanuni zake zinatambua uwepo wa mfumo huu wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi.

Katika miaka 16 ya utekelezaji wa usimamizi shirikishi Tanzania, Wizara yenye dhamana ya Uvuvi imefanikisha kuanzishwa kwa mfumo unaounganisha wanajamii na Serikali katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi kupitia vikundi vya BMUs ambavyo huanzishwa kwa hiari. Katika mfumo huu, wanajamii ndiyo watumiaji na wanufaika wa kwanza wa rasilimali za uvuvi. Aidha, katika mfumo huu BMUs zinakubaliana na Serikali kusimamia rasilimali hizo kupitia Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja (CFMAs) au Mitandao ya vikundi hivyo. Wizara yenye dhamana ya Uvuvi, kwa kushirikiana na wadau wa uvuvi, inasimamia na kutathmini Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usimamizi Shirikishi. Halmashauri za wilaya/ Manispaa/Jiji kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji na Mitaa zina jukumu la kushauri na kuelekeza utendaji wa majukumu ya BMUs.

### 2.1 Wadau na Majukumu yao katika Usimamizi Shirikishi

Wadau katika usimamizi shirikishi wa raslimali za uvuvi ni pamoja na Serikali Kuu (Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, TAMISEMI),

Halmashauri za Wilaya/Manispaa, Serikali za Vijiji/Mitaa na BMU. Aidha, wadau wengine ni pamoja na mashirika na taasisi zisizo za kiserikali (mfano: WWF-Tanzania, Sea Sense , Mradi wa Tuungane (Ziwa Tanganyika) nk), taasisi za utafiti, makampuni binafsi, watumiaji na jamii kwa ujumla. Majukumu ya wadau mbalimbali yatakuwa kama ifuatavyo:-

### 2.1.1 Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi

Majukumu ya vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi ni pamoja na:

a) Kuandaa Katiba kulingana na mahitaji ya mwongozo huu;
b) Kusimamia rasilimali za uvuvi katika maeneo yao;
c) Kuandaa na kutekeleza Mpango-Mkakati wa Usimamizi wa Dago na wavuvi wageni kulingana na mipango ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi kiwilaya na kitaifa;
d) Kupanga na kutekeleza mipango kazi ya robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima na bajeti zake kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na kuripoti matokeo ya utekelezaji wake;
e) Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za uvuvi pamoja na sheria ndogo za uvuvi za halmashauri husika, kijiji/mtaa;
f) Kushiriki katika kukusanya takwimu za uvuvi na utafiti wa uvuvi;
g) Kusimamia na kuhakikisha usafi wa mialo, bandari na masoko ya uvuvi yaliyo katika eneo la mtaa/kijiji ;
h) Kushiriki katika usajili wa wavuvi na zana zao pamoja na vyombo kwa kutoa mapendekezo ya awali na kukagua vyombo na zana za uvuvi kama zinakubalika kisheria ;
i) Kuwadhamini wanachama wake wanaoomba kusajili au kuongeza muda wa leseni na vibali vinavyohusika kwenye uvuvi na mazao yake;

j) Kuhakikisha na kuhamasisha wavuvi wote wanalipa ada ya leseni kwa wakati;
k) Kutunza rasilimali za kikundi ikiwa ni pamoja na daftari la usajili la wanachama, mali, kumbukumbu, taarifa ikiwa ni pamoja na takwimu za uzito, thamani na bei ya samaki katika mialo;
l) Kusimamia rasilimali za uvuvi katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ushiriki wa wanajamii katika maamuzi yanayowahusu;
m) Kutatua mizozo/migogoro baina ya wanachama, au baina ya vikundi zinavyohusika na usimamizi au uendelezaji wa rasilimali na mazingira ya uvuvi;
n) Kuelimisha wanachama na jamii juu ya masuala mbalimbali ya uvuvi na kusambaza taarifa za uvuvi kwa wadau;
o) Kushiriki katika michakato mbalimbali ya kisera na kisheria katika ngazi ya kijiji, kata, na wilaya husika;
p) Kushirikiana na Serikali ya Kijiji/Mitaa na wananchi katika kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo zinazolinda rasilimali za uvuvi na mazingira;
q) Kushirikiana na Serikali ya Kijiji/Mitaa, wadau wengine na wananchi kutayarisha Mipango ya Usimamizi ya Uvuvi katika ngazi ya Kijiji/Mtaa
r) Kushirikiana na BMUs zingine, Serikali za Vijiji/Mitaa, Watendaji wa Kata na Viongozi wengine katika ngazi mbalimbali kuunda Mtandao wa BMUs na maeneo ya usimamizi wa pamoja (CFMAs);
s) Kutayarisha taarifa za utekelezaji na kuziwasilisha kwenye Serikali ya Kijiji, Mtandao wa BMU katika Kata na Afisa Uvuvi wa Kata/Wilaya;
t) Kukusanya taarifa za takwimu mbalimbali za uvuvi katika maeneo wanayosimamia (taarifa za doria, taarifa za kiasi cha raislimali kilichovuliwa na takwimu nyingine za uvuvi);

u) Kuelimisha wanachama na wadau wengine kuhusu madhara ya matumizi ya zana haribifu pamoja na masuala yote ya uharibifu wa rasilimali za uvuvi na mazingira;
v) Kuandaa na kusimamia mikakati na mipango ya usimamimizi wa raslimali za uvuvi;
w) Kutayarisha na kutekeleza miradi ya maendeleo yenye kuzingatia uhifadhi wa  wa mazingira;
x) Kutekeleza kazi zingine kama itakavyoelekezwa na Mamlaka husika na kama BMUs zitakavyoona inafaa na kukubaliwa na Mamlaka.

### 2.1.2 Serikali za Vijiji/Mitaa

Majukumu ya Serikali za Vijiji/Mitaa ni pamoja na:

a) Kushirikiana na vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
b) Kusimamia uanzishwaji wa BMUs
c) Kupokea mapendekezo ya sheria ndogo kutoka kwa vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
d) Kusimamia na kuhakikisha utendaji wa vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi unafuata sheria;
e) Kushiriki katika kuunda Mtandao wa BMUs;
f) Kushirikiana na BMUs katika kuanzisha maeneo ya usimamizi ya pamoja;
g) Kushirikiana na BMUs katika kuandaa mipango ya usimamizi ya rasilimali za uvuvi;
h) Kufuatilia na kufanya tathmini ya maendeleo ya BMUs; na
i) Kupokea mapendekezo kutoka BMUs kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

### 2.1.3 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Halmashauri za Wilaya/Manispaa/Jiji zitatekeleza majukumu yafuatayo:

a) Kusimamia na kutekeleza Sheria na Kanuni za Uvuvi;
b) Kusimamia uanzishwaji na utendaji wa BMUs;
c) Kusimamia uanzishwaji na utendaji wa Mtandao wa BMUs katika maeneo yao;
d) Kupitisha sheria ndogo za vijiji/mitaa zinazohusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
e) Kuwezesha BMUs kuandaa na kutekeleza mipango ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
f) Kusimamia mipango na uanzishwaji wa maeneo ya usimamizi wa pamoja ya uvuvi (CFMAs);
g) Kutoa elimu ya ugani kuhusu uvuvi endelevu;
h) Kufuatilia ukusanyaji wa takwimu za uvuvi;
i) Kuwezesha BMUs kitaalamu, kisheria, kifedha na kusimamia rasilimali za uvuvi;
j) Kutayarisha mipango na mikakati ya muda mfupi na mrefu ya sekta ya uvuvi;
k) Kuwezesha BMUs kuwa na mfumo endelevu wa mapato yatakayowezesha utekelezaji wa mipango ya usimamizi wa uvuvi na mazingira;
l) Kufuatilia utekelezaji wa mipango na mikakati ya BMUs na CFMAs inayohusiana na usimamizi wa uvuvi; na
m) Kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za uvuvi na kuyagawa ipasavyo kwa kuzingatia kanuni na miongozo kama ilivyoidhinishwa; na
n) Kuunda kamati ya ushauri itakayohusisha wataalamu wa uvuvi, sheria, misitu, wanyamapori, maji, maendeleo ya jamii kwa lengo la kuzishauri BMUs na kutatua migogoro.

### 2.1.4 Sekretariet za Mikoa

Majukumu ya Sekretariet za Mikoa ni pamoja na:

a) Kusimamia halmashauri katika utekelezaji wa Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya uvuvi kwa kuzingatia sera ya ugatuaji wa madaraka;
b) Kushiriki katika kupitia Sera, Sheria na Kanuni za uvuvi;
c) Kushiriki katika kuandaa miongozo mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake; na
d) Kushiriki katika kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya uvuvi katika Halmashauri zao.

### 2.1.5 Ofisi ya Rais TAMISEMI

Majukumu ya OR-TAMISEMI ni pamoja na:

a) Kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya uvuvi na wadau wengine katika kusimamia rasilimali za uvuvi nchini;
b) Kushirikiana na Wizara husika katika kuwezesha BMUs kuwa na mfumo endelevu wa mapato;
c) Kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya uvuvi kuratibu mtandao wa BMUs;
d) Kushiriki katika kupitia Sera, Sheria na Kanuni za uvuvi;
e) Kushiriki katika kuandaa miongozo mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazingira yake;
f) Kupitisha Sheria ndogo zinazoandaliwa na Halmashauri;
g) Kuimarisha mawasiliano, ushirikiano na maelewano na wadau;
h) Kusaidia katika ukusanyaji na upatikanaji wa takwimu za uvuvi.
i) Kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza Sheria na Kanuni za uvuvi

### 2.1.6 Wizara yenye dhamana ya Uvuvi

Majukumu ya Wizara yenye dhamana ni pamoja na

a) Kutayarisha na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo ya Uvuvi ;
b) Kutayarisha mipango ya muda mfupi na mrefu ya maendeleo ya uvuvi;
c) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya uvuvi;
d) Kusimamia Sheria na Kanuni za Uvuvi;
e) Kutoa mafunzo kwa watumishi na wadau wengine kwenye mambo yahusuyo utunzaji, uhifadhi, maendeleo na matumizi endelevu na usimamizi wa rasilimali ya uvuvi;
f) Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi;
g) Kushirikiana na nchi pamoja na taasisi na mashirika ya kikanda na kimataifa katika kusimamia shughuli za uvuvi;
h) Kuimarisha ushirikiano wa BMUs za Tanzania na za nchi nyingine;
i) Kuandaa mwongozo wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi;
j) Kutathmini utendaji wa kazi za BMUs;
k) Kukusanya takwimu na taarifa za uvuvi;
l) Kushirikishana taarifa na wadau na kusaidia shughuli za ugani.
m) Kushiriki katika usimamizi wa uvuvi kwa kutoa elimu kwa wananchi na BMUs;
n) Kutoa msaada wa kifedha na kitaaluma ili kufanikisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
o) Kutoa huduma za ugani kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji/ Mitaa;
p) Kuhamasisha wadau wengine kushiriki katika shughuli za uvuvi.

### 2.1.7 Wadau wa Maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali

Majukumu ya wadau wa Maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali ni pamoja na :


a) Kushirikiana na Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwenye usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi.
b) Kushiriki katika kuunganisha na kuzileta pamoja sekta zinazoshabihiana na sekta mtambuka.
c) Kushiriki , kuwezesha na kujengea uwezo wadau kuhusu:
i) Dhana ya usimamizi shirikishi kuanzia ngazi ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamiikwa ujumla
ii) Kutengeneza mazingira wezeshi katika usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi
iii) Kuwezesha utafiti
iv) Kusaidia katika kutoa mafunzo na uelewa
v) Kushiriki katika kuandaa mbinu wezeshi za kuinua na kuboresha maisha ya jamii
d) Kushiriki katika kutunga, kuandaa na maboresho ya Sera, Sheria, Kanuni na miongozo ya Sekta ya Uvuvi hususani usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi
e) Kuwezesha wadau wa sekta katika utekelezaji wa dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kifedha na kitaaluma.
f) Kushiriki katika kuinua na kuboresha teknolojia na uvumbuzi katika usimimizi wa rasilimali za uvuvi.
g) Kuwezesha na kuendeleza ushiriki wa makundi maalum katika dhana ya usimamizi shirikishi
h) Kushiriki na kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi

## 2.2 Mahusiano na Mawasiliano Miongoni mwa Wadau

Ili kufikia malengo ya usimamizi shirikishi mahusiano miongoni mwa wadau hayana budi kuboreshwa na kufafanuliwa. Mwongozo huu umebainisha majukumu ya wadau muhimu wa usimamizi shirikishi katika kielelezo Namba 1;

Mtiririko wa usambazaji wa taarifa miongoni mwa wadau umeonesha katika kielelezo namba 1. Utoaji na usambazaji wa taarifa za Kiserikali kwa wadau uzingatie taratibu za utoaji wa taarifa za Serikali.

**Kielelezo Na. 1:** Mtiririko wa usambazaji wa taarifa miongoni mwa wadau



# 3.0 TAASISI YA USIMAMIZI SHIRIKISHI KATIKA NGAZI YA JAMII

## 3.0 TAASISI YA USIMAMIZI SHIRIKISHI KATIKA NGAZI YA JAMII

Mfumo wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika ngazi ya jamii utaendeshwa kitaasisi ili kuhakikisha malengo ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi ngazi ya kijiji/mtaa yanafikiwa. Mfumo huo utazingatia kuwepo kwa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa rasilimali za uvuvi BMUs ambavyo vitaanzishwa katika ngazi za vijiji/mitaa. Taasisi hizo za Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi katika ngazi ya jamii zitaanzishwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi zilizopo. Taasisi hizi zitaundwa kwa lengo la kulinda, kutunza, kuendeleza na kusimamia raslimali za uvuvi na mazingira yake kwa kushirikiana na wadau wengine, ikiwemo Serikali.

### 3.1 Vikundi vya Usimamizi Shirikishi

Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi katika ngazi ya jamii vitakuwa ni taasisi huru za kiraia zilizoundwa na wanajamii waliojiunga kwa pamoja kwa nia ya kushiriki katika usimamizi wa uvuvi katika mtaa/kijiji (mtaa/mitaa, kijiji/vijiji), na ambao wanajishughulisha kwa njia moja au nyingine na kazi za uvuvi, zinazoendesha au kutegemea uvuvi. Kwa mujibu wa sheria na kanuni za uvuvi zilizopo vikundi hivi vitasajiliwa. Vikundi vitapaswa kufuata taratibu zote za usajili ikiwemo kuwa na katiba.

### 3.2 Muundo wa Kikundi cha Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU)

Kikundi cha Usimamizi Shirikishi kitakuwa na muundo wa taasisi ya kiraia ambao utafafanuliwa na katiba ya BMU husika. Aidha, kipindi cha uongozi kitakuwa kama ilivyoainishwa katika kanuni za uvuvi.

BMU itakuwa na viongozi wafuatao:-

a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti;
b) Katibu na Katibu Msaidizi;
c) Mweka hazina
d) Mzee Maarufuanayekubalika

BMU itakuwa na kamati 3 ambazo zitakuwa na idadi ya wajumbe kama ifuatavyo:-

a) Kamati ya Usafi wa Mazingira, Udhibiti na Doria – Wajumbe 5
b) Kamati ya Takwimu na taarifa – Wajumbe 5
c) Kamati ya Fedha na Uzalishaji Mali – Wajumbe 5

Aidha, BMU inaweza kuunda Kamati nyingine zisizozidi mbili (2) kama itakavyopendekezwa, na kuridhiwa na Mkutano Mkuu wa BMU kulingana na mahitaji na Katiba ya BMU ili mradi majukumu yake hayaingiliani na kamati zilizopo. Viongozi wa BMU na Wajumbe wa kamati za BMU watachaguliwa na Mkutano Mkuu kwa kupigiwa kura baada ya kuomba nafasi hizo. Kila Kamati itakuwa na Mwenyekiti na Katibu. Katiba za BMU zinatakiwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira, Tanzania.

## 3.3. Vyombo Vikuu vya Kikundi cha Usimamizi Shirikishi

Muundo wa uongozi wa BMU utakuwa na Mkutano Mkuu, Kamati Tendaji, na Kamati ndogo kama vyombo vya utekelezaji wa majukumu ya BMU ya kila siku.

### 3.3.1 Mkutano Mkuu

Mkutano Mkuu utakuwa ndicho chombo cha juu kabisa cha maamuzi na wajumbe wake watakuwa ni wanachama wote wa BMU. Mkutano Mkuu utaidhinisha mipango ya maendeleo ya BMU, matumizi ya

fedha pamoja na kazi nyingine kama itakavyofafanuliwa na Katiba ya BMU. Mkutano Mkuu utafanyika kila baada ya miezi sita au wakati wowote kutakapokuwa na dharura.

Majukumu ya Mkutano Mkuu wa BMU ni:-

i) Kutoa maamuzi ya mwisho kwa masuala yote yanayohusu taasisi;
ii) Kuteua, kuchagua na kuridhia au kukataa uchaguzi/uteuzi wa kiongozi au mjumbe wa kikundi husika;
iii) Kuidhinisha mipango yote ya taasisi ikiwemo: Mipango ya Usimamizi wa rasilimali za uvuvi na mazingira; Mipango ya Maendeleo; Mipango kazi; na Makubaliano baina ya Taasisi na taasisi nyingine.
iv) Kuidhinisha miradi ya kiuchumi, matumizi ya taasisi pamoja na taarifa za ukaguzi wa Mahesabu;
v) Kuidhinisha mabadiliko ya Katiba au sehemu ndani ya muundo wa BMU

### 3.3.2 Kamati Tendaji

Kutakuwa na Kamati Tendaji yenye wajumbe wasiopungua tisa na wasiozidi 11 waliochaguliwa kidemokrasia na Mkutano Mkuu. Mwenyekiti wa BMU atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Kamati Tendaji na Katibu wa BMU atakuwa Katibu wa Kamati Tendaji. Wajumbe wengine wa Kamati Tendaji ni kama ifuatavyo; Makamu Mwenyekiti; Katibu Msaidizi; Mhazini; Mzee Maarufuanayekubalika; na Wenyeviti wa Kamati za Kamati Udhibiti na Doria; Kamati ya Takwimu na taarifa. Ikiwa Mkutano Mkuu utaongeza kamati nyingine, mwenyekiti wa kamati hiyo atakuwa mjumbe wa Kamati Tendaji.

Kamati Tendaji, pamoja na majukumu mengine yaliyoainishwa kwenye katiba ya BMU itakuwa na majukumu yafuatayo:-

a) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za BMU katika eneo/kijiji/mtaa husika;
b) Kusimamia, kulinda na kuhifadhi rasilimali za uvuvi na mazingira;
c) Kusimamia uvunaji na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira;
d) Kuandaa Mpango Mkakati, Mpango wa Usimamizi na Mpango Kazi kwa ajili ya kusimamia shughuli za uvuvi katika maeneo yao na kufuatilia utekelezaji wake na kuuwasilisha kwa mkutano mkuu kwa kujadiliwa na kupitishwa;
e) Kusimamia na kuratibu ukusanyaji wa mapato ya BMU na matumizi yake;
f) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi za BMU kwenye Mkutano Mkuu na katika ngazi ya kijiji, kata, wilaya, jiji na manispaa;
g) Kubuni Mikakati ya usimamizi wa rasilimali na mazingira ya uvuvi na kuishauri Halmashauri ya kijiji/mtaa juu ya utekelezaji wake;
h) Kupendekeza kwa Serikali ya Kijiji majina ya wavuvi wanaostahili kupewa leseni za vyombo, zana za uvuvi pamoja na leseni za biashara ya mazao ya uvuvi kwa kushirikiana na Maafisa Uvuvi ili kuhakikisha kuwa wanaopewa leseni wameshajiandikisha kuwa wajumbe wa BMU;
i) Kuteua maeneo ya mazalia ya samaki na kupendekeza maeneo yenye matumizi maalum kwa kutumia elimu asilia yenye ushauri wa kisayansi na kutoa mapendekezo ya aina ya usimamzi/mkakati wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi;
j) Kuimarisha mtandao wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa raslimali za uvuvi ili kufanikisha upashanaji wa habari na taarifa ulio thabiti (mfano biashara, udhibiti wa majina ya

wavuvi waharibifu, uwekaji wa bei za samaki na mazao yake unaozingatia haki), usimamizi ya wa rasilimali za uvuvi na usalama wa watu na mali zao; na

k) Kusimamia usafi wa mazingira na ubora wa mazao ya samaki kwenye forodha/mialo.

### 3.3.3 Kamati ndogo:

Ili kurahisisha utendaji, BMU itaunda kamati ndogo zisizopungua tatu na zisizozidi tano zitakazoshughulikia maeneo mahususi ya utekelezaji. Kamati ndogo zitajumuisha:

a) Kamati ya Usafi wa Mazingira, Udhibiti na Doria
b) Kamati ya Takwimu na taarifa
c) Kamati ya Fedha na Uzalishaji Mali

Wajumbe wa kamati hizi watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa BMU kwa kuzingatia vigezo vitakavyowekwa na kupitishwa na Katiba ya BMU.

#### 3.3.3.1 Kamati ya Usafi wa Mazingira, Udhibiti na Doria

Pamoja na kazi nyingine zilizoainishwa kwenye Katiba ya BMU husika, Kamati ya Usafi wa Mazingira, Udhibiti na Doria itakuwa na majukumu yafuatayo;-

a) Kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya uvuvi kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji/Mtaa;
b) Kukagua na kuweka kumbukumbu za wavuvi wageni na zana zao na kutoa kibali cha kuingia kwenye bandari/mialo na makambi kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji/Mtaa;
c) Kutoa mapendekezo kuhusu wavuvi, vyombo na wasafirishaji wanaoomba leseni za uvuvi, leseni na vibali vya usafirishaji wa mazao ya uvuvi;

d) Kutunza kumbukumbu zinazohusu taarifa za doria na udhibiti kwa kushirikiana na Katibu wa BMU;

e) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi za kamati kwenye Kamati Tendaji;

f) Kudhibiti ubora wa mazao ya uvuvi;

g) Kusimamia usafi wa mialo/bandari na mazingira; na

h) Kutoa makadirio ya idadi ya wavuvi wanaoweza kufanya shughuli zinazohusiana na uvuvi kwenye mialo/forodha za kijiji na kuwasilisha mapendekezo kwenye Serikali ya Kijiji.

#### 3.3.3.2 Kamati ya Takwimu na Taarifa

Pamoja na kazi nyingine zilizoainishwa kwenye katiba ya BMU, Kamati ya Takwimu itakuwa na majukumu yafuatayo;-

a) Kuratibu kazi za ukusanyaji wa takwimu za uvuvi wa kila siku na sensa ya uvuvi;

b) Kutunza takwimu za wavuvi wa Kijijini/Mtaa;

c) Kusaidia katika tafiti mbalimbali za kibaiolojia na kijamii;

d) Kufuatilia na kuripoti maendeleo ya utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya usimamizi kwa Kamati Tendaji;

e) Kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa kazi za kamati kwenye Kamati Tendaji,na

f) Kufanya marejesho ya matokeo ya taarifa za uvuvi zinazokusanywa.

#### 3.3.3.3 Kamati ya Fedha na Uzalishaji Mali

Pamoja na kazi nyingine zilizoainishwa kwenye Katiba ya BMU husika, Kamati ya Fedha na Uzalishaji Mali itakuwa na majukumu yafuatayo;-

a) Kuratibu upatikanaji wa fedha za kuendesha shughulli za BMU;

b) Kusimamia Mikataba na makubaliano ya utekelezaji yanayohusu BMUs;

c) Kuratibu ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vilivyoainishwa na BMU;
d) Kubuni vyanzo vya mapato ya BMU na kutoa mapendekezo kwa Kamati Tendaji;
e) Kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa kazi kwa Kamati Tendaji; na
f) Kushauri Kamati Tendaji kuhusu matumizi na mapato ya BMU.

## 3.4 Majukumu na Wajibu wa Viongozi wa BMU

Pamoja na majukumu mengine yaliyoainishwa kwenye Katiba za BMU Majukumu na wajibu wa Viongozi wa BMU yatakuwa kama ifuatavyo;-

### 3.4.1 +Mwenyekiti wa BMU

a) Atakuwa ndiye kiongozi na Msimamizi Mkuu wa BMU;
b) Ataongoza Mkutano Mkuu na mikutano ya Kamati Tendaji;
c) Atakuwa ndiye Msemaji Mkuu wa BMU; na
d) Ataidhinisha malipo yote ya fedha za BMU yaliyopitishwa na Kamati Tendaji
e) Atakuwa msimamizi mkuu wa fedha na mali za BMU.

### 3.4.2 Katibu wa BMU

a) Atakuwa mtunza kumbukumbu mkuu wa BMU husika,
b) Atapokea kumbukumbu kutoka kwa makatibu wa kamati ndogo, Mweka hazina na Boharia kwa lengo la kuweka kumbukumbu za BMU husika vizuri;
c) Ataandaa mikutano baada ya kuwasiliana na Mwenyekiti, na kuandika taarifa za mikutano;
d) Atatunza kumbukumbu za mikutano ya kamati, na nyaraka za BMU;

e) Ataandaa taarifa za kazi za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka na kuziwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa BMU;
f) Atatunza kumbukumbu za wajumbe wa BMU, wavuvi, na wadau husika wa uvuvi; na
g) Ataandaa taarifa ya makabidhiano ya uongozi wa BMU na mali za BMU.

### 3.4.3 Mweka hazina

a) ;
b) Kutunza kumbukumbu za fedha na vitabu vya hesabu za BMU husika;
c) Kupokea na kuweka fedha taslimu katika akaunti ya benki ya BMU;
d) Kutunza rejista ya wanachama waliolipa ada na michango mbalimbali
e) Kutunza vifaa vyote vinavyohusiana na ofisi ya Mweka hazina;
f) Kuandaa taarifa za fedha za mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka pamoja na taarifa nyingine za fedha zitakazohitajika na kuziwasilisha kwenye Mkutano wa Mkuu wa BMU;
g) Kupokea mahitaji ya fedha na kuwasilisha kwenye kamati tendaji;
h) Kuandaa na kufanya malipo yaliyoidhinishwa na Mwenyekiti wa BMU husika kama yalivyopitishwa na Kamati Tendaji
i) Kuwasilisha taarifa ya mapato namatumizi ya BMU husika kwenye Kamati Tendaji na Mkutano Mkuu wa BMU;

### 3.4.4 Boharia

a) Atapokea nakutunza mali za BMU husika
b) Kupokea maombi ya mikopo, na kuandaa mahitaji ya ofisi na vifaa;
c) Kuandaa na kutunza kumbukumbu, risiti, mikopo na vifaa viliyotolewa kwenye bohari;

d) Kuwasilisha taarifa za bohari kwa Katibu wa BMU husika ambaye ataiwasilisha kwenye Kamati Tendaji na Mkutano Mkuu wa BMU; na

### 3.4.5 Mzee Maarufu naanayekubalika

a) Kushauri uongozi katika masuala mbalimbali yahusuyo uvuvi, maadili, utawala na usimamizi;
b) Kushiriki katika vikao vya Mkutano Mkuu wa BMU na Kamati Tendaji; na
c) Kushiriki katika kusuluhisha migogoro ndani ya BMU husika.

## 3.5 Utaratibu wa Ukusanyaji Fedha na Matumizi

BMU inapaswa kuwa na vyanzo vya fedha ambavyo pamoja na vyanzo vingine vitakuwa ni michango ya ada ya uanachama ambayo italipwa kila mwaka. Kiwango cha ada kitabainishwa na katiba ya BMU husika. Pia, kila mwanachama anayetaka kujiunga na BMU itamlazimu kutoa kiingilio ambacho kitatolewa mara moja tu. Vyanzo vingine vya mapato vitaainishwa katika Katiba ya BMU.

### 3.5.1 Ukusanyaji wa Fedha

Ukusanyaji wa fedha za BMU utafanywa na Mweka hazina kwa kusimamiwa na Kamati Tendaji. Masharti yafuatayo yatazingatiwa:-

a) Fedha zote ni lazima zikatiwe risiti ya malipo;
b) Malipo yatapokelewa na Mweka hazina . Endapo Mweka hazina hatakuwepo malipo yatapokelewa na Katibu au mjumbe aliyeteuliwa na Kamati Tendaji;
c) Kutakuwepo na rejista/daftari ya wanachama waliolipa michango ambayo itatunzwa na katibu Michango yote iliyopokelewa lazima kutolewa taarifa kwenye Kamati Tendaji na Mkutano Mkuu wa BMU;

Masharti haya yatapokiukwa wahusika watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria za nchi na Katiba ya BMU.

### 3.5.2 Matumizi ya Fedha

Bajeti ya BMU ya kila mwaka itaandaliwa na Kamati Tendaji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa BMU. Kamati Tendaji itaidhinisha kiasi cha fedha kulingana na Katiba ya BMU.
Utaratibu wa kutumia fedha utakuwa kama ifuatavyo:-

a) Kutakuwa na fomu maalumu ya maombi ya fedha (fomu A) itakayotakiwa kupitishwa na Mwenyekiti na Katibu wa BMU pamoja na Mweka hazina ;
b) Utoaji fedha benki utahitaji kutiwa saini na watu watatu; Mweka hazina , Mjumbe mmoja kutoka Kamati ya Takwimu ya BMU na Mwenyekiti wa BMU;
c) Taarifa ya maandishi itaandaliwa na kutolewa kwa kila matumizi yatakayofanyika;

## 3.6 Ukomo wa Uanachama wa BMU

Uanachama katika BMU utakoma kutokana na sababu zifuatazo:-

a) Iwapo mwanachama atashindwa kuhudhuria mikutano mara tatu mfululizo pasipo sababu yoyote au bila kutoa taarifa ya mdomo au kwa maandishi ya yeye kushindwa kuhudhuria mkutano;
b) Iwapo atashindwa kulipa ada na michango yake ya kila mwaka na michango mbalimbali bila sababu ya msingi kwa mujibu wa katiba husika;
c) Iwapo atakwenda kinyume na matakwa ya katiba husika;
d) Iwapo mwanachama atafariki au kama ataugua ugonjwa wowote utakaomfanya ashindwe kutimiza majukumu yake

kwa kwa kipindi cha mwaka mmoja;

e) Iwapo mwanachama ataamua kujitoa kwa hiari yake mwenyewe;

f) Akipatikana na hatia ya kuvunja sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa uvuvi;

g) Akipatikana na makosa ya jinai

h) BMU haitarejesha ada na michango yoyote iliyotolewa na mwanachama aliyekoma uanachama kwa sababu yoyote.

# 4.0 MCHAKATO WA UANZISHAJI WA BMU

## 4.0 MCHAKATO WA UANZISHAJI WA BMU

### 4.1 Mahali na Eneo la Utawala wa BMU

Kikundi cha Usimamizi Shirikishi kitaanzishwa katika ngazi ya kijiji/ mtaa na itabidi kisajiliwe katika mamlaka inayohusika kwa kufuata taratibu za sheria na kanuni za uvuvi. Kila BMU itakuwa na eneo la uvuvi wanalolisimamia kwa kuzingatia mipaka inayotambuliwa rasmi na Serikali ya Kijiji/Mtaa, Halmashauri ya Wilaya/Minispaa/ Jiji. BMUs inaweza kushirikiana na kijiji/mtaa, wilaya, mkoa na Serikali Kuu katika kusimamia shughuli zake na katika ushirikiano, wanachama wa BMU moja wanaweza kufanya kazi nje ya mipaka yao ya kijiji/mtaa.

Sifa ya kijiji/mtaa kuanzisha BMU ni kuwa na eneo la maji ya asili/ bwawa ambalo lina rasilimali za uvuvi zitakazosimamiwa.

**Angalizo:**

1. Ikitokea Kijiji/Mtaa ambao kuna shughuli ya uvuvi, na ambapo wakazi wa kijiji/mtaa huo hawajishughulishi na kazi hiyo, BMU itaundwa na watumiaji wa rasilimali za uvuvi wanaotumia eneo hilo kwa kusimamiwa na serikali ya kijiji/mtaa husika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitathibitisha;
2. Wavuvi wanaotoka kijiji/mtaa jirani ambavyo havina eneo la maji ya asili/bwawa ambalo lina rasilimali za uvuvi zitakazosimamiwa, wavuvi toka maeneo hayo watatakiwa kujiunga na BMUs za jirani na kufuata taratibu za BMU husika.

## 4.2 Hatua za Kuanzisha BMU

Uanzishwaji wa BMU utafuata utaratibu ufuatao:-

### 4.2.1 Hatua ya kwanza: Kujenga uelewa na kukuza mwamko wa jamii

Uanzishwaji wa BMU utaanza kwa kuhamaisha wanajamii umuhimu wa kushiriki katika usimamizi shirikishi wa raslimali za uvuvi. Kazi hii ya kuhamasisha wanajamii itafanywa na Mamlaka za Serikali ya Mitaa, Serikali ya Kijiji na kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali au mashirika ambayo yanajishughulisha na uvuvi na ambayo yako tayari kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya uvuvi. Njia mbalimbali zinaweza kutumika kufikisha ujumbe huu kutegemeana na mazingira ya kijiji/mtaa husika kwa mfano mikutano, semina, mabango na vipeperushi.

Wanajamii waliotayari kuanzisha BMUs watatakiwa kuandaa katiba ya BMU na kufuata taratibu za usajili wa BMUs kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za uvuvi.

### 4.2.2 Hatua ya pili: Uchaguzi wa Viongozi wa BMU

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri atatangaza tarehe ya uchaguzi wa BMU katika Halmashauri yake na pia atakuwa msimamizi Mkuu katika zoezi zima la uchaguzi wa viongozi wa BMUs.

Kipindi cha kuchukua fomu za maombi ya nafasi mbalimbali kitakuwa siku thelathini (30). Uchaguzi utafanyika baada ya siku thelathini (30) kabla ya siku ya uchaguzi ambao utafanyika katika Mkutano Mkuu wa wanachama wote. Mamlaka za Serikali za Mtaa (Serikali ya Kijiji/Mtaa) zitathibitisha ukazi wa waliojiandikisha kuunda BMU kwa kutumia daftari la kudumu la wakazi. Aidha, itahakiki na

kujiridhisha iwapo idadi ya waliohudhuria kwenye uchaguzi kama wamefikia asilimia 65 ya waliojiandikisha kwa ajili ya kuunda BMU. Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ataandaa na kusimamia uchaguzi wa viongozi wa BMU.

### 4.2.2.1 Sifa za Mgombea wa Uongozi wa BMU

Mwanachama yoyote anayetaka kugombea uongozi ndani ya BMU atalazimika kuwa na sifa zifuatazo:

a) Awe raia wa Tanzania;
b) Awe mkazi wa eneo husika kwa zaidi ya miaka miwili na awe hajahamisha makazi yake wakati wa kufanya uchaguzi;
c) Awe na umri usiopungua miaka 18;
d) Awe mwaminifu na mwenye akili timamu;
e) Aweze kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili;
f) Awe na elimu ya msingi (darasa la saba);
g) Awe hajawahi kuhukumiwa kwa makosa yanayohusu uvuvi na jinai;
h) Asiwe kiongozi wa chama cha siasa;
i) Asiwe mfanyakazi wa Serikali;
j) Awe na wadhamini angalau watatu ambao ni wanachama wa BMUs inayoanzishwa.

### 4.2.2.2 Angalizo Kuhusu Uchaguzi wa Viongozi wa BMU:

a) Mtu mmoja asidhamini zaidi ya mgombea mmoja;
b) Mkutano Mkuu wa wanachama waliojiandikisha kuunda BMU utachagua viongozi wa BMU pamoja na kamati mbalimbali za BMU;
c) Upigaji wa kura utakuwa ni wa siri;
d) Kila mgombea atamteua wakala mmoja (1) ambaye atahusika katika kuhesabu na kuhakiki kura; na
e) Mgombea atakuwa mwangalizi katika kuhesabu kura.

### 4.2.2.3 Muda wa Uchaguzi

Uchaguzi utaanza saa mbili asubuhi hadi saa saba kamili mchana. Kura zitaanza kuhesabiwa mara baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika. Matokeo ya uchaguzi yatatangazwa na Mtendaji wa Kijiji kabla ya saa kumi kamili jioni siku hiyo hiyo ya uchaguzi.

### 4.2.2.4 Rufaa katika Uchaguzi wa BMU

Mgombea yeyote ana haki ya kutokukubali matokeo yaliyotangazwa na msimamizi wa uchaguziendapo hajaridhika na matokeo, na ana haki ya kukata rufaa kwa kufuata taratibu zifuatazo:-

a) Ajaze fomu ikiambatana na barua ya rufaa ikieleza sababu za kutokubali matokeo yaliyotangazwa na kuwasilisha kwa Mtendaji Kata ndani ya masaa ishirini na nne (24) baada ya matokeo kutangazwa;(fomu ziandaliwe)
b) Mtendaji Kata atapokea fomu na barua ya rufaa na kuweka kumbukumbu ya tarehe na saa ya kupokea rufaa hiyo;
c) Mtendaji Kata kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji/mitaa mingine pamoja na Afisa Uvuvi wa Kata watajadili ili kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa;
d) Maamuzi ya rufaa yatatolewa ndani ya kipindi cha siku saba (7) toka siku ya kuwasilishwa rufaa kwa Mtendaji wa Kata ; na
e) Mgombea asiporidhika na uamuzi uliotolewa na Mtendaji Kata, atakata rufaa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/Jiji ambaye atatoa uamuzi wa mwisho.

### 4.2.2.2 Makabidhiano ya Uongozi baada ya Uchaguzi

Taratibu zifuatazo zitatumika katika makabidhiano ya uongozi kwa BMU ambayo awamu ya utawala wake umefikia kikomo:-

a) Kiongozi anayemaliza muda wake atatakiwa kuandaa taarifa yake kwa kipindi chote alipokuwa madarakani;

a) Makabidhiano yafanyike ndani ya kipindi cha siku saba (7) mara baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa au pale ambapo kuna rufaa baada ya rufaa kukamilika na uamuzi kutangazwa;
b) Afisa Uvuvi kwa kushirikiana na Mtendaji wa Kijiji/Mtaa watasimamia makabidhiano ya uongozi na mali za BMU kwa uongozi mpya;
c) Katibu wa BMU aliyechaguliwa atapokea na kutunza kumbukumbu za makabidhiano ya uongozi pamoja na mali za BMU; na
d) Makabidhiano yatakamilika kwa pande zote mbili kujaza na kusaini fomu yenye kuainisha mali zote za BMU.(fomu husika itengenezwe)

### 4.2.3 Utaratibu wa Kuandaa Katiba ya BMU

Wanachama waliokwisha unda BMU wataandaa Katiba ya BMU kwa kufuata taratibu za usajili wa BMUs kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi. Aidha, Mamlaka za Serikali za Vijiji/Mitaa zitasaidia BMUs katika kuandika Katiba. Maudhui ya Katiba ya BMU yatajumuisha vipengele vifuatavyo:-

a) Jina la BMU
b) Anuani na mahali BMU ilipo
c) Eneo la usimamizi
d) Malengo ya BMU
e) Kijiji au Vijiji vinavyounda BMU
f) Sifa za wajumbe
g) Muundo na majukumu ya watendaji
h) Sifa za viongozi
i) Muda wa kuongoza
j) Makabidhiano ya ofisi
k) Mfumo wa uwakilishi
l) Uwajibikaji wa BMU kwa Kijiji/Mtaa

m) Mahusiano na Halmashauri ya vijiji
n) Vyanzo na usimamizi wa fedha
o) Utatuzi wa migogoro
p) Adhabu
q) Ukomo wa uwepo wa BMU

Angalizo: Maudhui ya Katiba yasipingane na maudhui ya Sheria, Kanuni za uvuvi na Mwongozo huu.

### 4.2.4 Hatua ya Tatu: Kusajili BMU na kufungua Akaunti

Baada ya kutengeneza Katiba, uongozi uliochaguliwa utakuwa na jukumu la kuisajili BMU kwa Mkurugenzi wa Uvuvi ambaye ndiye Mamlaka ya usajili ya vikundi vya BMUs nchini. Aidha, nakala ya Hati ya usajili wa BMU itawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya/Manispaa/Jiji kwa uthibitisho. Hatimaye hatua za ufunguaji wa akaunti zitafuata.

# 5.0 UENDESHAJI WA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA UVUVI

## 5.1 Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi (CFMA)

Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi ni eneo ndani ya maji ya kitaifa lenye mipaka ya kijiografia ambayo itaainishwa kwa mujibu wa utaratibu uliooneshwa kwenye mwongozo huu, na ambalo limeidhinishwa na Mkurugenzi wa Uvuvi kuwa linasimamiwa na BMU zaidi ya moja kwa madhumuni ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi na kuhimiza matumizi yake kwa busara. Maeneo haya yataainishwa na kutambuliwa rasmi baada ya kufanyiwa utafiti wa mwenendo wa uvuvi na mipaka ya mifumo mikuu ya kiikolojia.

Vigezo vya kufuata katika kuteua vijiji vitakavyounda Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi vitajumuisha:-

a) Kuwepo kwa BMUs katika vijiji husika;
b) Kuwepo kwa eneo la uvuvi ambalo linatumiwa na kijiji zaidi ya kimoja; na
c) Jamii kupitia mabaraza ya BMUs kuonesha utayari wa kushirikiana katika kuanzisha Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi kwenye Eneo la Pamoja.

## 5.2 Utaratibu wa kufuata katika kuanzisha Maeneo ya Pamoja ya Usimamizi wa Uvuvi

Sheria ya Uvuvi inaruhusu taasisi za usimamizi wa uvuvi kuungana kwa lengo la kusimamia eneo la maji linalotumika kwa shughulli za uvuvi. Eneo la usimamizi litakaloainishwa na kusimamiwa na BMU zaidi ya moja litaeleweka kama ni Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi. Uanzishwaji Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi utafuata hatua zifuatazo:-

### 5.2.1 Hatua ya Kwanza: Utafiti shirikishi wa uvuvi wa eneo linalotarajiwa kusimamiwa

Lengo kuu la hatua hii ni kukusanya taarifa ambazo zitatumika kuongoza mchakato wa kupanga usimamizi na kulitathmini eneo

na rasilimali iliyomo. Utafiti huu unaweza ukafanywa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Mamlaka za Wilaya au mbia mwingine yeyote kama vile Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Sehemu kuu za utafiti huu ni kama ifuatavyo:

a) Mfumo wa kuvua katika Jamii. Huu ni utafiti wa awali ambao unalenga kutoa taarifa za msingi zitakazotumika kuainisha masuala yatakayojadiliwa katika hatua za awali na mpango wa utafiti wa kina.

b) Utambuzi wa kina wa mwenendo wa Uvuvi na maeneo ya uvuvi: Utafiti huu una hatua tatu;

    i. Hatua ya kwanza: Utafiti wa majadiliano na wanajamii kutambua mchango wa uvuvi katika jamii na uendeshaji wa uvuvi wa wageni na wenyeji, maeneo muhimu ya uvuvi na muingiliano wa wavuvi katika maeneo hayo.
    ii. Hatua ya pili: Kuainisha maeneo ya uvuvi yaliyotajwa kwenye utafiti wa kwanza, kwa kuyatembelea na kuchukua alama zake za Longitude na latitude.
    iii. Hatua ya tatu: Kufanya utafiti wa zana za uvuvi zinazotumiwa na wajanamii wa vijiji husika.

c) Tathmini ya rasilimali: Utafiti huu unakusudia kutoa taarifa za msingi ambazo zitaelekeza uundaji wa mpango wa usimamizi na kutoa kipimo (reference) kwa ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini ya ufanisi wa usimamizi wa rasilimali za uvuvi.

### 5.3.2 Hatua ya Pili: Mashauriano na Uhamasishaji

Hatua hii inalenga kutambulisha wazo la uanzishwaji wa Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi kwa wadau. Mdau yeyote anaweza akawasilisha wazo hili kwa wadau wengine. Hatua hii itakuwa na vipengele vifuatavyo:-

a) Uhamasishaji wa Jamii: Jamii zitakazohusika katika utayarishaji wa eneo la pamoja zitahamasishwa kupitia njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara juu ya haja ya kuwa na usimamizi wa pamoja baina yao na majirani zao.

b) Mashauriano miongoni mwa washiriki: Wadau wa uvuvi, Halmashauri ya Kijiji na taasisi nyingine za kijamii katika kijiji/mtaa na hata watu binafsi watashauriana kuhusu uanzishwaji wa maeneo ya usimamizi wa pamoja wakiangalia faida na hasara za kuingia usimamizi wa pamoja baina ya jamii na jirani zao ambao wanatumia maeneo ya pamoja ya uvuvi.

c) Kuwasilisha taarifa ya makubaliano kwenye mkutano mkuu wa kijiji/mtaa: Baada ya mashauriano miongoni mwa washiriki, taarifa ya makubaliano juu ya uanzishwaji wa maeneo ya usimamizi wa pamoja itawasilishwa kwenye Mkutano wa Kijiji/Mtaa kwa ajili ya kupata ridhaa.

d) Kuomba idhini: Jamii za wavuvi zitaomba idhini ya kuunda maeneo ya usimamizi wa pamoja kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika. Taasisi mojawapo ya washirika au Kamati ya muda inayoundwa na taasisi zinalenga kuungana, itatuma ombi ikieleza dhamira ya kuanzisha eneo hilo na taasisi watakazoshirikiana nazo kwenye eneo hilo.

### 5.3.3 Hatua ya Tatu: Uanzishaji wa Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi

a) Baada ya kuruhusiwa na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika, Taasisi zitaunda Kamati ya Uratibu ya Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi itakayohusisha wajumbe toka BMUs zote husika.

b) Kamati ya Uratibu wa Usimamizi wa Pamoja itakutana kuainisha mipaka ya Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi kwa mashauriano na vijiji/mitaa jirani, taasisi zao; na chini ya usimamizi wa Afisa Mtendaji wa Kata, na Afisa Uvuvi wa Wilaya husika. Wadau wengine wanaweza kushauri uteuzi wa eneo hili.

c) Baada ya kuridhiana na washiriki wengine, Kamati ya uratibu itawasilisha ripoti ya maelezo (au ramani); ripoti za mikutano zilizosainiwa, na Mkataba wa Makubailiano baina ya taasisi shiriki inayoonesha eneo la usimamizi na mipaka yake kwa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa.

### 5.3.4 Hatua ya Nne: Kutengeneza Mpango wa Usimamizi

Hatua hii inahusisha utengenezaji wa mpango wa usimamizi na mipango kazi ya eneo la usimamizi. Kamati ya Uratibu ya eneo la usimamizi itaandaa Mpango wa Usimamizi na hatimaye Mpango-kazi. Mambo muhimu katika hatua hii ni kama ifuatavyo:-

a) Kuleta uwiano wa Mipango ya Usimamizi, na Mipango-kazi ya BMU;

b) Kuainisha na kuziba mapengo katika mikakati ya usimamizi ya BMU kwa mtazamo wa Eneo la Pamoja la Usimamizi wa Uvuvi;

c) Kutengeneza Mpango kazi wa enao la usimamizi wa pamoja.

### 5.3.5 Hatua ya Tano: Kuomba Ridhaa kwa Mkrugenzi wa Uvuvi

Baada ya kupata ridhaa ya Mamlaka ya Halmashauri husika kamati itaomba kuingia Mkataba wa usimamizi wa maeneo ya pamoja kwa Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uvuvi.

## 5.4 Uratibu wa Kitaasisi katika Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi

Uratibu wa usimamizi shirikishi katika maeneo ya usimamizi wa pamoja utaanza mara baada ya kupata ridhaa ya Mkurugenzi wa Uvuvi. Dhana ya kuwepo kwa usimamizi wa pamoja inatokana na ukweli kuwa; Jamii za wavuvi wamekuwa wakitumia maeneo ya uvuvi kwa ushirikiano baina ya vijiji mbalimbali tangu asili na hivyo vijiji vina haki ya matumizi na hivyo vina wajibu wa kushiriki katika usimamizi wake. Pia, bahari, maziwa, mito na mabwawa yanayo mifumo ya kiikolojia ambayo mara nyingi huwa inavuka mipaka ya maeneo ya vijiji/mitaa, wilaya na hata mikoa. Usimamizi shirikishi utaratibiwa katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:

1. **Ngazi ya Kitaifa - Wizara yenye dhamana ya uvuvi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI**

    i) Kusimamia maendeleo ya usimamizi shirikishi wa uvuvi katika kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi na mazingira;

    ii) Kuongoza shughuli za mfumo wa Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

2. **Ngazi ya Mikoa – Sekretarieti ya Mkoa**

    i) Kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia maendeleo ya usimamizi shirikishi wa uvuvi katika kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za uvuvi na mazingira;

    ii) Kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia maeneo ya usimamizi wa pamoja kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na uvuvi.

## 3. Ngazi ya Wilaya: Mamlaka ya Serikali za Mitaa

i) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maeneo ya pamoja;
ii) Kujenga uwezo wa Kamati za Uratibu wa maeneo ya usimamizi wa pamoja kwa kutoa mafunzo, maelekezo na ushauri katika nyanja mbalimbali za utekelezaji wa kazi za usimamizi shirikishi;
iii) Kuidhinisha mipango ya usimamizi ya maeneo ya usimamizi wa pamoja iliyomo ndani ya wilaya;
iv) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa BMU na Kamati za Uratibu wa Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja; na
v) Kutayarisha na kutoa ripoti za maendeleo ya usimamizi shirikishi kwa vipindi vya robo mwaka na kuziwasilisha Idara ya Maendeleo ya Uvuvi.

## 4. Ngazi ya Katakatika Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja

Taasisi za Uratibu wa shughuli za usimamizi wa Maeneo ya Pamoja zitafanya kazi zifuatazo:

i) Kuleta uwiano wa mipango ya usimamizi ya vijiji kutoka BMUs ili kurahisisha shughuli za uratibu;
ii) Kuratibu mikakati ya usimamizi wa raslimali inayotumiwa na BMU zilizomo ndani ya eneo la pamoja;
iii) Kujenga uwezo wa BMUs katika nyanja za rasilimali, mafunzo na vitendea kazi;
iv) Kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuendeleza shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika eneo husika;

v) Kuzishauri BMUs na Halmashauri za Wilaya juu ya masuala yanayohusiana na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi, aina ya viumbe wanaohitaji uhifadhi, ufuatiliaji wa uvuvi; na

vi) Kuunganisha BMUs na Mamlaka za Serikali za Mitaa na vijiji kupitia mabaraza ya kata.

**i. Ngazi ya Kijiji/Mtaa - BMU**

BMUs zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kushirikiana na BMUs na Kamati ya Uratibu katika usimamizi wa pamoja;

ii) Kutekeleza kazi kulingana na mipango ya usimamizi na mipango-kazi ya pamoja,

iii) Kutekeleza maelekezo yanayotoka kwenye Kamati ya Usimamizi wa Pamoja, Mamlaka ya Halmashauri na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi;

iv) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti za utekelezaji kwa Kamati ya Uratibu na Afisa Mtendaji wa Kijiji.

## 5.5 Kamati ya Uratibu

Kamati ya Uratibu itaundwa na wajumbe watano (5) watakaochaguliwa miongoni mwa wajumbe wenye dhamana za kiofisi ndani ya BMU husika. Wajumbe watakaounda Kamati ya Uratibu watakuwa ni:

- Mwenyekiti
- Makamu Mwenyekiti
- Katibu
- Mweka hazina
- Mratibu wa Vikosi-kazi

## 5.6 Uchaguzi wa Uongozi wa Kamati ya Uratibu

Uchaguzi wa viongozi wa Kamati ya Uratibu utafanywa kwa kuzingatia ngazi za uongozi. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watachaguliwa kutoka kati ya Wenyeviti wa BMUs, vivyo hivyo Katibu atachaguliwa kutoka kati ya Makatibu wa BMUs. Mweka hazina atachaguliwa miongoni mwa watunza hazina wa BMUs.

Uchaguzi wa viongozi utaratibiwa na Katibu Tarafa wa kila Tarafa. Endapo uchaguzi utahusisha zaidi ya Tarafa moja, Afisa Uvuvi wa Wilaya kwa kushirikiana na Makatibu Tarafa husika wataamua mahala na tarehe ya uchaguzi.

Kulingana na Sheria ya Uvuvi na Mwongozo wa BMU, Viongozi wa Kamati ya Uratibu watakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitatu na kuchaguliwa tena mara moja tu. Wakati muhula wa madaraka ya viongozi wa BMU unaisha, Viongozi wa Kamati ya Uratibu watakuwa madarakani hadi hapo Kamati Tendaji mpya ya BMU itakaposimikwa. Endapo mihula ya madaraka ya uongozi wa BMU na Kamati ya Uratibu itatofautiana, Katibu Tarafa kwa kushauriana na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji watahakiki uteuzi wa viongozi mbadala.

## 5.7 Kazi za Kamati ya Uratibu

Kazi za Kamati ya Uratibu zitajumuisha:-

a) Kutunza nyaraka na kumbukumbu za CFMA ikiwa ni pamoja na: Nyaraka za Makubaliano na taasisi nyingine; Kumbukumbu za utekelezaji wa kazi; Kumbukumbu za Vikao.
b) Kupitia Mpango wa Usimamizi na Mipango-Kazi na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu BMU husika kwa kuidhinishwa;
c) Kutatua migogoro kati na baina ya BMUs;
d) Kusimamia utawala bora;

e) Kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji maduhuli na kuhakikisha ugawaji sahihi wa fedha baina ya BMUs;
f) Kusimamia upatikanaji wa takwimu na taarifa za uvuvi;
g) Kufuatilia uendeshaji wa makambi/dago ya uvuvi;
h) Kufuatilia na kushauri kamati za BMU kuhusiana na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za usimamizi shirikishi. (mchango wa BMU kwenye CFMA kazi hii iwekwe kwenye majukumu BMU)

## 5.8 Utaratibu wa usimamizi wa uvuvi ndani ya Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja

### 5.8.1 Utayarishaji wa Mpango wa Usimamizi

Uongozi wa Taasisi ya Usimamizi Shirikishi utaandaa Mpango wa Usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwa kushirikiana na Watendaji wa Vijiji, Mtendaji wa Kata, wataalamu wa ngazi ya halmashauri ya wilaya na Asasi za maendeleo zilizopo. Mpango huu utaainisha vipaumbele vya masuala muhimu ya uvuvi na mazingira yanayowagusa wanajamii na kupanga mikakati ya kuitatua.

Mpango wa Usimamizi wa eneo la pamoja utatayarishwa kwa kuwianisha Mipango ya Usimamizi ya BMUs husika na kubuni mikakati ya usimamizi wa maeneo ya uvuvi. Mchakato wa kuwianisha utafuata hatua zifuatazo:

a) Kamati ya uratibu itatayarisha rasimu ya Mpango wa Usimamizi uliowianishwa kwa kutumia mipango ya BMUs;
b) Rasimu ya Mpango ya eneo la pamoja itapitiwa na kila Mkutano Mkuu wa BMU kwa kuidhinishwa;
c) Kamati ya Uratibu itapokea na kupitia mapendekezo na kuyajumuisha katika Rasimu ya Mpango wa eneo la pamoja endapo itakubalika;
d) Rasimu itawasilishwa tena kwa Kamati Tendaji ya BMU kwa ajili ya uboreshaji zaidi; na

e) Mpango wa mwisho uliowianishwa utawasilishwa kwa kila BMU ili upitishwe na kutekelezwa.

Mpango wa Usimamizi utakuwa ni kwa kipindi cha miaka mitano.

### 5.8.2 Utayarishaji wa Mpango kazi

a) Kamati ya Uratibu itatayarisha Mpango Kazi wa mwaka uliowianishwa kutokana na Mipango Kazi ya BMUs;
b) Mpango Kazi wa mwaka utapitishwa na Mkutano Mkuu wa BMU;
c) Kamati ya Uratibu itaratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa mwaka uliowianishwa kama chombo cha uratibu.

## 5.9 Usimamizi wa Makambi (Madago) ya Uvuvi

Sheria ya Uvuvi nchini Tanzania inatambua uvuvi wa kuhamahama. Katika uvuvi wa kuhamahama wavuvi hutengeneza makambi/dago kwa ajili ya makazi ya muda mfupi. Uvuvi katika makambi/madago husimamiwa kwa kutumia mwongozo wa makambi ya uvuvi ambao umeweka maelekezo na taratibu za uvuvi katika maeneo waliopo.

Mwongozo huu unawezesha vijiji kupanga utaratibu utakaowawezesha watumiaji wa kambi za uvuvi kuendesha shughuli zao kwa ufanisi, amani na usalama kwa kufuata Sheria zinazosimamia usalama wa nchi, maendeleo ya uvuvi na utunzaji wa mazingira. Sheria hizo zinajumuisha Sheria na Kanuni za Uhamiaji, Sheria na Kanuni za Uvuvi, Sheria ndogo (By-laws) za Wilaya, Vijiji na taratibu nyingine za vijiji husika.

# 6.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na tathmini ni upimaji na uhakiki wa maendeleo ya utekelezaji wa usimamizi shirikishi kwa kuangalia ufanisi, fursa na changamoto za utekelezaji kwa lengo la kuboresha utendaji.

## 6.1 Ngazi za ufuatiliaji

Ufuatiliaji utafanywa katika ngazi zifuatazo:

a) Ngazi ya Taifa: Ufuatiliaji utafanywa na Wizara yenye dhamana ya uvuvi kwa kushirikiana na wizara zinazohusiana na Sekta ya Uvuvi.
b) Ngazi ya Serikali za Mitaa: Ufuatiliaji utafanywa na Halmashauri husika.

Wadau watafanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na vyombo vya Serikali kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wanajamii.

## 6.2 Maeneo Makuu ya Viashiria vya Ufuatiliaji

Viashiria vitakavyotumika katika ufuatiliaji ni kama ifuatavyo:-

a) Uwezo wa vikundi shirikishi kujiendesha na kushiriki katika usimamizi shirikishi
b) Uwezo wa kukusanya na kusimamia fedha
c) Kiwango cha ufanisi wa utekelezaji wa viashiria vya mipango ya usimamizi ya BMU na CFMA
d) Tathmini ya mabadiliko ya viashiria vya hali ya rasilimali kama vile upatikanaji wa samaki, hali ya mazingira n.k.
e) Mabadiliko ya hali ya kiuchumi ya wanajamii

## 6.3 Njia za ufuatiliaji

Njia za ufuatiliaji zitakazotumika kupima maendeleo ya vikundi shirikishi ni pamoja na:-

a) Kusoma taarifa mbalimbali;
b) Kuandaa mikutano katika ngazi mbalimbali;

c) Kukagua maeneo na shughuli za uvuvi shirikikishi kwa nyakati tofauti;
d) Kuwa na watoaji wa taarifa katika ngazi mbalimbali; na
e) Kutumia mitandao ya kijamii.

Taarifa zitakazokusanywa zitajumuisha taarifa za mikutano ya BMU katika ngazi mbalimbali, ushiriki wa BMU katika maamuzi ya ndani na nje ya kijiji, taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali kama vile Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi, Mpango wa Usimamizi wa Makambi na kadhalika; matokeo ya ufuatiliaji wa takwimu za uvuvi, sensa ya zana za uvuvi na hali ya rasilimali; na matokeo ya dodoso nyingine zinazohoji hali halisi ya kijamii au kama itakavyohitajika.

Ili kuwa na ufuatiliaji wenye tija, BMU zitahitajika kuwa na:

a) Watu wenye ufahamu na ujuzi;
b) Uelewa wa dhana ya ushirikishwaji;
c) Uelewa wa dhana ya ufuatiliaji, umiliki wa rasilimali na uthubutu wa kutenda;
d) Utunzaji wa kumbukumbu sahihi; na
e) Uwepo wa zana za kukusanyia taarifa.

## 6.4 Tathmini

Tathmini ya Usimamizi shirikishi itazingatia vipengele vifuatavyo:- viashiria vitakavyofanyiwa tathmini, muda wa kufanya tathmini, matokeo na uendelevu wa usimamizi shirikishi.

Tathmini zitafanywa katika ngazi mbalimbali, kulingana na mahitaji rasilimali fedha na watu:

a) BMUs zitafanya tathmini ya hali ya eneo la usimamizi kabla ya mpango kuanza kutekelezwa ili kupata hali halisi ya awali kabla ya kuanza utekelezaji.
b) BMU zitafanya tathmini ya maendeleo ya usimamizi shirikishi kwa kuangalia utendaji wao;
c) Halmashauri zitafanya tathmini ya maendeleo ya usimamizi shirikishi kwa kuangalia utendaji wa BMUs, CFMA na mitandao yao katika wilaya na matokeo yake;
d) Serikali kuu itafanya tathmini ya usimamizi shirikishi ikiwa ni sehemu ya kuboresha utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uvuvi katika eneo hili.
e) Wadau wengine pia, wanaweza kufanya tathmini za usimamizi shirikishi.

## 6.5 Matokeo ya Tathmini

Mwongozo huu unamtaka kila mdau atakayefanya tathmini kuwasilisha matokeo ya tathmini yake kwa wadau wengine katika ngazi ya Jamii, Wilaya na Wizara na kwa lugha itakayoeleweka kwa wadau husika.

Tathmini itapima vigezo vifuatavyo:

a) Uwezo wa vikundi shirikishi kujiendesha na kushiriki katika usimamizi shirikishi;
b) Uwezo wa kukusanya na kusimamia fedha;
c) Kiwango cha utekelezaji wa viashiria vya mipango ya usimamizi ya BMU;
d) Mabadiliko (chanya au hasi) ya viashiria vya hali ya rasilimali (upatikanaji wa samaki, hali ya mazingira n.k.); na
e) Mabadiliko ya hali ya kiuchumi ya wanajamii.

Maelekezo ya ufuatiliaji wa usimamizi shirikishi yameoneshwa katika Jedwali Namba 1 - 4.

**Jedwali Na. 1:** Uwezo wa vikundi shirikishi kujiendesha na kushiriki katika usimamizi shirikishi

| Kipimo | Njia ya kupima | Muda |
|---|---|---|
| Idadi ya Mikutano Mikuu ya BMU | Idadi ya mihutasari na mahudhurio ya wanachama katika mikutano | Kama ilivyoaninishwa na mwongozo |
| Idadi ya Mikutano ya Kamati Tendaji | Taarifa ya mahudhurio ya wanachama | Kama ilivyoaninishwa na mwongozo |
| Mikutano ya Kamati ndogo | Taarifa ya mahudhurio ya wajumbe | Kama ilivyoainishwa na mwongozo |
| Ushiriki wa BMU katika shughuli za kijamii | Taarifa ya Ushiriki | Kama ilivyoaninishwa na mwongozo |
| Idadi ya migogoro | Taarifa za utatuzi wa migogoro | Kama itakavyojitokeza |

**Jedwali Na. 2:** Uwezo wa kukusanya na kusimamia fedha

| **Kipimo** | **Njia ya kupima** | **Muda** |
|---|---|---|
| Mabadiliko ya asilimia/ kiwango cha fedha kutokana na bajeti za ndani | Mapato yanayokusanywa | Miezi sita/12 |
| Asilimia ya mapato inayotokana na vyanzo vya ndani | Mapato ya vyanzo vya ndani kugawa kwa mapato yote | Miezi sita/12 |
| Asilimia ya matumizi yaliyofanyika | Ripoti ya fedha ya BMU/Vikundi Shirikishi | Miezi sita/12 |
| Matumizi sahihi ya fedha | Hati safi | Miezi 12 |

**Jedwali Na. 3:** Mabadiliko (chanya au hasi) ya viashiria vya hali ya rasilimali (upatikanaji wa samaki, hali ya mazingira n.k.)

| **Kipimo** | **Njia ya kupima** | **Muda** |
|---|---|---|
| Mavuno na nguvu ya uvuvi | Takwimu za Uvuvi mwaloni/bandarini | Kwa mwezi |
| Hali ya Matumbawe | Takwimu za ufuatiliaji | Kwa mwaka |
| Matukio ya uvuvi wa mabomu | Takwimu za ufuatiliaji | Kwa mwezi |
| Uvuvi Haramu (makokoro, n.k.) | Taarifa ya zana zilizokamatwa | Robo mwaka |

**Jedwali Namba 4:** Mabadiliko ya hali ya kiuchumi ya wanajamii

| Kipimo | Njia ya kupima | Muda |
|---|---|---|
| Mapato (fedha) kutokana na mauzo ya samaki | Takwimu za uvuvi mwaloni/bandarini | Kwa mwezi |
| Matumizi ya bidhaa muhimu za kujikimu maisha kutokana na mapato ya uvuvi na | Umiliki wa bidhaa na samani | Kwa mwaka |
| Matumizi katika huduma za kijamii (elimu, afya nk) kutokana na mapato ya uvuvi | Taarifa za maendeleo ya jamii | Miezi sita |

## 6.6 Ufuatiliaji na Tathmini wa Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja

Ufuatiliaji na tathmini utahusisha ukusanyaji wa taarifa na takwimu utakaofanywa na BMUs mara kwa mara. Lengo kuu la kufuatilia utendaji ni kupima mabadiliko yatokanayo na hatua za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika eneo husika. Kazi zinazofanywa na BMUs zitafuatiliwa na Kamati ya Uratibu na Mamlaka za Wilaya au mdau mwingine yeyote ili kuhakikisha madhumuni ya usimamizi wa pamoja wa eneo la uvuvi yanafikiwa.

### 6.6.1 Madhumuni ya Ufuatiliaji na Tathmini

Madhumuni ya ufuatiliaji na tathmini ni pamoja:-

a) Kutoa taarifa kwa ajili ya kupima maendeleo, utendaji na matokeo ya usimamizi wa pamoja wa uvuvi;

b) Kuchangia upatikanaji wa takwimu za uvuvi; na

c) Kuboresha usimamizi wa maeneo ya pamoja ya uvuvi kwa maendeleo ya rasilimali za uvuvi.

### 6.6.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini ni moja ya kazi za kila siku katika utekelezaji wa kazi za BMUs na hivyo itaunganishwa na kuwa sehemu ya Mpango wa Usimamizi na Mpango Kazi. Ufuatiliaji na Tathmini utafanyika katika maeneo makuu yafuatayo:

a) Takwimu za aina ya mazao ya uvuvi na kiwango cha uzalishaji;
b) Takwimu za idadi ya wavuvi, zana na vyombo vya uvuvi;
c) Takwimu ya wadau muhimu katika sekta ya uvuvi katika eneo husika;
d) Takwimu za utekelezaji wa sheria za uvuvi na sheria ndogo zilizopitishwa na Halmashauri ili kuangalia ufanisi na changamoto zilizojitokeza;
e) Takwimu za aina ya migogoro inayojitokeza;
f) Taarifa za utendaji kazi za BMU na Mitandao yake;
g) Ripoti za vikao vya BMU;
h) Taarifa ya mapato na matumizi ya BMU;
i) Taarifa za doria, zana haramu na wahalifu walio kamatwa;
j) Idadi ya wanachama wa BMU walioko katika eneo husika.

**Jedwali Na. 5:** Viashiria vya Maendeleo ya Usimamizi wa Uvuvi wa Pamoja

| Kazi | Viashiria |
|---|---|
| Ufuataji wa sheria | • Idadi ya doria (safari na muda)<br>• Idadi ya zana haramu za uvuvi zilizosalimishwa au kushikwa<br>• Matukio ya uhalifu yaliyokutwa au yaliyoripotiwa<br>• Idadi ya wahalifu waliokamatwa<br>• Idadi ya kesi zilizopelekwa mahakamani, hatua zilizochukuliwa na matokeo<br>• Idadi ya wajumbe wa BMUs wanaotimiza wajibu wao<br>• Uwiano wa idadi ya wavuvi wenye leseni na wasiokuwa na leseni<br>• Idadi ya vyombo vya uvuvi vyenye leseni na usajili na vile visivyo na leseni<br>• Upungufu wa migogoro katika jamii |
| Ukusanyaji wa mapato ya BMU | • Fedha zilizopatikana kutoka vyanzo mbalimbali<br>• Utunzaji wa kumbukumbu za fedha |
| Matumizi ya fedha za BMU | • Matumizi kulingana na kazi zilizopitishwa<br>• Utunzaji wa kumbukumbu za matumizi |
| Sensa ya uvuvi na miundombinu | • Idadi ya vyombo vya uvuvi<br>• Idadi ya wavuvi, wachakataji, wauzaji nk<br>• Idadi ya zana za uvuvi na vifaa vingine |
| Kufanya usafi katika mialo, kambi na vyombo vya uvuvi | • Kupungua kwa magonjwa ya kuambukiza<br>• Mifumo ya ukusanyaji na uhifadhi wa taka ngumu<br>• Uwepo wa vyoo<br>• Uwepo wa maji safi na salama<br>• Kuwepo kwa vifaa vya kubebea samaki<br>• Kuwepo kwa bidhaa za kuhifadhia samaki (barafu nk) |
| Ushiriki wa wadau katika kazi za Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja | • Idadi ya wajumbe wa BMU (wanaume/wanawake) waliojihusisha kwa kila aina ya kazi<br>• Idadi ya wabia wengine waliojihusisha na kila aina ya kazi<br>• Idadi ya wajumbe wa kamati waliojihusisha kwa kila kazi<br>• Idadi ya mikutano ya kamati iliyoendeshwa<br>• Idadi ya wageni na Maafisa waliotembelea BMU |

### 6.6.3 Ufuatiliaji wa hali ya rasilimali

Shughuli za aina hii zinahusu ufuatiliaji wa idadi ya rasilimali ya samaki na kiwango cha ikolojia kilichopo katika makazi yao (mfano matumbawe). Ufuatiliaji wa rasilimali utalenga kufahamu aina mbalimbali za samaki na kiasi cha samaki kwa kutumia mbinu za kisayansi, ili kujua kipato kinachotokana na samaki katika kila mtumbwi, kupima urefu na uzito wa samaki. Ufuatiliaji wa rasilimali ya msingi iliyopo utahitaji kutathmini mazingira ya makazi na makuzi ya samaki yaliyopo ndani ya maji pamoja na mabadiliko ya jamii za samaki. Viashiria katika ufuatiliaji wa aina hii vimeoneshwa katika jedwali la 6;

**Jedwali Na. 6: Viashiria vya ufuatiliaji wa hali ya rasilimali**

| Kazi | Viashiria |
|---|---|
| Mapato na nguvu ya uvuvi | • Kiasi (uzito), aina na thamani ya samaki walioshushwa mwaloni<br>• Idadi ya safari za kuvua katika eneo kwa kipindi cha muda maalum |
| Mahudhurio katika kambi/mwalo za uvuvi | • Idadi ya wavuvi wanaokwenda kwenye kambi/mialo ya uvuvi kwa kila kijiji na eneo la mavuvi<br>• Uwiano wa idadi ya wavuvi wa kambi/mwalo kwa kila aina ya shughuli<br>• Idadi ya wavuvi katika kambi/mwalo kwa aina ya zana na vyombo<br>• Muda wa makazi katika kambi/mwalo kwa aina ya zana za uvuvi na kijiji watokako |

### 6.6.4 Kutoa Ripoti

Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini zitaunganishwa katika taarifa za BMUs za kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na mwaka zikionesha:

- Maendeleo ya kazi za BMUs dhidi ya madhumuni/malengo;
- Hali ya rasilimali na mwenendo wa uvunaji dhidi ya rasilimali ya msingi iliyopo;
- Hali ya aina muhimu za samaki;
- Changamoto za Usimamizi na mafunzo; na
- Mapendekezo

## 6.7 UTAFITI

Mwongozo huu unatambua umuhimu wa ushiriki wa vikundi vya usimamizi shirikishi katika tafiti mbalimbali za maendeleo ya uvuvi, kijamii, mazingira na ikolojia katika maeneo yao. Ushiriki huu unaweza kujumuisha vikundi shirikishi pekee au kwa ushirikiano na watafiti wengine (TAFIRI, FETA, Vyuo Vikuu, Watafiti wa kujitegemea n.k). Maeneo ya utafiti yanaweza kujumuisha ushiriki wa vikundi vya usimamizi shirikishi katika kutambua na kuanzisha maeneo ya usimamizi wa pamoja, maeneo nyeti kimazingira, ubunifu katika usimamizi na kuendeleza rasilimali ya uvuvi.

Mdau yeyote anaweza kufanya utafiti kwa kufuata taratibu zilizopo, ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini au kuchangia kwenye tasnia ya sayansi kwenye usimamizi na maendeleo ya uvuvi kwa ujumla. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huo hayana budi kurejeshwa kwa wadau na kwa lugha yenye kueleweka kwa walengwa wakiwemo jamii za wavuvi ili kuleta uelewa wa masuala muhimu ya usimamizi shirikishi.

Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi vinaweza kubaini maeneo ya utafiti katika maeneo yao. Aidha, maeneo yatakayobainishwa na kukubalika yatajadiliwa na wajumbe katika Mkutano Mkuu wa BMU ili kuridhiwa.

**KIAMBATISHO (FOMU A)**
**KIKUNDI CHA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA RASILIMALI ZA UVUVI**

**BMU YA ...........................................**
**KIJIJI/MTAA...................................**
**WILAYA..........................................**
**S.L.P...............................................**

TAREHE........................

FOMU YA MAOMBI YA FEDHA (FOMU A)

1. Nawasilisha maombi ya Fedha T. Shilingi...................................
...........................(Maneno).......................................(Tarakimu)
2. Jina la muombaji ...........................................(Sahihi)................
3. Cheo cha Muombaji ...............................................................

**<u>KIBALI</u>**

4. Maombi yako ya TSHs.........................................Yamekubaliwa/ Yamekataliwa
5. Sababu ya kukataliwa...............................................................
.......................................................................................

**<u>MAPENDEKEZO</u>**

6. Imependekezwa upewe TSHs ..................................(Tarakimu)
.......................................................................................
7. Lengo la Fedha zilizoombwa:-

7.1...............................................................TSHS............................
7.2...............................................................TSHS...........................
7.3...............................................................TSHS...........................
7.4...............................................................TSHS...........................

7.5.............................................................TSHS..........................
7.6.............................................................TSHS..........................
7.7.............................................................TSHS..........................
7.8.............................................................TSHS..........................
7.9.............................................................TSHS..........................
7.10...........................................................TSHS..........................

**JUMLA TSHS....................................**

**KUIDHINISHA FEDHA**

8. Jina la Mwenyekiti wa BMU.............................Sahihi..................
9. Jina la Mtunza Hazina.....................................Sahihi..................
10. Jina la Mjumbe (Mtia Saini).............................Sahihi..................
11. Jina la Mpokeaji...........................................Sahihi..................
12. Malipo yamefanywa kwa njia ya Fedha Taslimu/Hundi/ Vocha Na.....................................

**NB: (a) Fomu hii lazima isainiwe na 8, 9 na 10 hapo juu;**
**(b) Lazima iambatishwe na muhtasari wa kikao wa Kamati Tendaji/Ndogo ulio idhinisha matumizi/utoaji wa fedha tajwa.**